# Nipashe

Jumanne Agosti 6, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581760

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




**PSG YAJITOSA RASMI KUMSAJILI ALVAREZ** UKURASA 21

UKURASA 2

**Waziri** ataka trafiki kuweka utaratibu mzuri kuepusha foleni

UKURASA 3



**Ajira** mpya 37,616 mbioni kutangazwa

UKURASA 19

**WHO** kufanya tathmini ya maambukizi ugonjwa Mpox

# TLS na LHRC zalaani vikali madai binti kubakwa

• **Zataka** wahusika wachukuliwe hatua, Askofu Mwamakula, Madeleka watoa neno ... *Ukurasa 3*



Peter Madeleka



Dk. Anna Henga



Boniface Mwabukusi




Mmoja wa wakazi wa Ifakara akiwa ameshika picha za Rais Samia Suluhu Hassan wakati wa mkutano wa hadhara katika Uwanja wa CCM Ifakara, Kilombero mkoani Morogoro jana. **PICHA: IKULU**

## NEMC yaja na mkakati kugeuza taka ngumu kuwa fursa kiuchumi

UKURASA 7

## Samia awapa mawaziri maagizo sita

UKURASA 2

**MICHEZO** **MUTALE AWATAKA YANGA, BALUA AAHIDI MABAO** UK.24

**MAONI,** UK.6

HABARI KITAIFA



Mjumbe wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Dk. Zakia Mohamed Bakar, akishuhudia Mkazi wa Mtaa wa Karyambwa wilayani Muleba mkoani Kagera, Vedastus Manya, akiboresha taarifa zake kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura katika kituo cha Shule ya Msingi Rubungo jana mkoani Kagera. Mikoa ya Kagera na Geita imeanza zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura na litaendelea hadi Agosti 11, mwaka huu. **PICHA: INEC**

# Rais Samia awapa mawaziri maagizo sita

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa maelekezo sita kwa mawaziri na viongozi wa Mkoa wa Morogoro ikiwamo kuacha kuwahamishia wananchi katika maeneo ya hifadhi kwa lengo la kupata uongozi.

Aidha, alikemea vitendo vya viongozi wanaowanyoya wakulima kwa kuongeza vipimo kwenye magunia ili wanunue kwa bei ya chini na kupata faida kubwa huku wazalishaji wakipata hasara.

Rais alitoa maelekezo hayo jana alipohutubia wananchi wa Ifakara, Wilaya ya Kilombero, akiwa katika ziara ya siku sita mkoani Morogoro kukagua miradi ya maendeleo na kutatua changamoto za wananchi.

Alisema kuna baadhi ya viongozi wanaofanya uwakala wa mazao kwa wakulima kwa njia zisizo sahihi kwa kuunganisha magunia mawili kisha kuwalazimisha wakulima wajaze debe kumi kwenye gunia moja ambayo ni zaidi ya kilo 150 na kununua kwa Sh. 80,000, bei ambayo si halali.

"Uwe diwani, uwe mwenyekiti wa kijiji, uwe ngazi yoyote, kama unafanya biashara hii ya kuongeza kipimo kwenye magunia ya mkulima na ukalipa kidogo ili wewe unufaike hufanyi haki," alisema.

Alisema wakulima wa mpunga wanatumia nguvu kubwa kuzalisha bidhaa hiyo hivyo anapotokea dalali na kununua kwa bei ndogo humnufaisha yeye na kumwacha mkulima katika umaskini.

"Sasa anapotokea mjanja na kudhulumu nguvu ya mkulima hii sio sawa, anayefaidi hapa ni mtu wa kati na si mkulima na familia waliopoteza nguvu zao," alisema.

Aliwaagiza viongozi wa mkoa na wilaya kusimamia wakulima wauze mazao kwa bei halali ili waweke akiba na kufanya shughuli zao bila kutegemea ruzuku kutoka serikalini.

Alimwagiza Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe kuhakikisha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) wanakwenda kununua mpunga moja kwa moja kwa wakulima kwa bei ya serikali ya Sh. 900 ili kuwaepusha na madalali wanonunua kwa Sh. 570.

Alisema serikali inaendelea kuikuza sekta ya kilimo kwa kuongeza miundombinu ya umwagiliaji ili wakulima wavune mara mbili kwa mwaka na sekta hiyo itoe ajira kwa vijana.

Aidha, alimwelekeza Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki, kudhibiti wananchi kuhamishwa katika maeneo ya hifadhi badala ya kusubiri wahamie na kutulia kisha kwenda kuwaondoa.

Alisema inapokaribia kipindi cha uchaguzi wanasiasa hasa madiwani wanapoona dalili za kukosa uongozi katika maeneo waliko wanawahamisha watu na kuanzisha makazi katika maeneo ya hifadhi kwa lengo la kupata wapigakura na maeneo ya kuongoza. Aliwataka wanasiasa hao kuacha tabia hizo kwa kuwa maeneo hayo yameandaliwa makusudi kwa ajili ya matumizi ya baadaye ya kuleta maendeleo ya nchi na kuhifadhi rasilimali.

"Vijiji vingi vilivyoanzishwa ndani ya maeneo ya hifadhi ni kwa ajili ya wanasiasa, iwe madiwani au wabunge, halafu ni hao hao wanaokuja kusimama kuwatetea watu walioingia ndani ya hifadhi hizo," alisema.

Aliwaomba wananchi wanaodai fidia kuiacha serikali imalize miradi ya maendeleo na ikishakamilisha itawalipa madai yao.

"Kwa hiyo tuacheni tufanye miradi, mambo ya fidia mimi nawahakikishia hatonyimwa mtu haki yake, tukiwa tayari tutalipa fidia," alisema.

Aliwasisitiza wananchi wa Ifakara kutunza mazingira hasa Mto Kilombero kwa kuacha kufanya shughuli za kibinadamu ikiwamo kulisha mifugo ili iwanufaishe wananchi wa maeneo mengi ya mkoa huo.

Alisema serikali itasimamia kuwa na umeme wa uhakika katika eneo hilo ili kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji wa viwanda na kuongeza thamani ya mazao yanayolimwa mkoani humo na kuwaletea maendeleo.

Aliwasisitiza wananchi wa mkoa huo kupeleka watoto shule kwa sababu serikali inatumia gharama kuwakalipia elimu ili kumwondolea mzazi mzigo na watoto wote waipate.

"Inasikitisha unapita kwenye ziara, saa za watoto kuwapo shule unakuta watoto wengi wanazubaa njiani na hawapo shule," alisema.

Alisema serikali inaendelea kufanya kazi kubwa kuboresha upatikanaji huduma za jamii ikiwamo kushughulikia changamoto za watumishi katika elimu na afya.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, alisema atatekeleza agizo alilopewa na rais la kushughulikia kero ya ushuru wa kubambikwa inayolalamikiwa na wananchi wa eneo hilo.

"Mheshimiwa Rais umenitaka leo hii (jana) nikae na wakurugenzi wote wa halmashauri, wawakilishi wa wananchi, wenyeviti wa halmashauri na mameya ili kwa pamoja tuzungumze tatizo hili ambalo linawakabili wananchi katika maeneo yetu haya," alisema.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alisema kama rais akiridhia, kuanzia mwezi huu serikali itaanza kununua mpunga kwa wakulima kwa bei ya Sh. 100,000 kwa gunia la kilo 150 sawa na Sh. 900 kwa kilo.

Alisema pia ameagiza kampuni zinazonunua mpunga kununua moja kwa moja kwa wakulima mashambani badala ya Morogoro mjini kwa madalali.

Aliagiza kushughulikia uwazi katika kupima kiwango cha sukari kwa kuruhusu mwakilishi wa wakulima na mataalamu kutoka Bodi ya Sukari kuingia na kuthibitisha kiwango ambacho mkulima amekisema.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alipiga marufuku vitendo vya watumishi wa mamlaka ya maji nchini ya kuwabambikia bili za maji watumiaji.

Aidha, alisema serikali ina mpango wa kuleta mita za maji za malipo ya kabla kama ilivyo umeme ili kuondoa changamoto ya kubambikiwa.

## Waziri ataka trafiki kuweka utaratibu kuepusha foleni maeneo ya ujenzi

**Na Maulid Mmbaga**

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, ametoa maelekezo kwa maofisa wa usalama barabarani kuhakikisha wanaweka utaratibu mzuri wa kuongoza na kuepusha msongamano wa magari wa muda mrefu katika maeneo ya ujenzi wa barabara za mwendokasi.

Akizungumza jana wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara za mwendokasi unaoendelea katika maeneo mbalimbali mkoani Dar es Salaam, Mhandisi Kasekenya alisisitiza trafiki kuzingatia mitembeo ya magari isibadilike na kama kutakuwa na changamoto kuwe na muda maalumu wa kuzifanya njia zifunguke.

Pia, alisema wameona kwenye maingilio ya kutoka katika Reli ya SGR kuja kwenye Barabara za Mwendokasi (DRT), yako maeneo ambayo sio rafiki kwa maana ya madaraja yalivyojengwa, akisisitiza makandarasi kutengeneza njia rafiki ili kuepusha ajali.

"Kama ni kupunguza miinuko wapunguze ama namna ya kuingia kutoka DRT kwenda kwenye barabara zinazovuka SGR, ni muhimu sana kuzijenga vizuri kwasababu zitakuwa ni 'high way' zitakuwa na mwendo wa haraka hivyo wananchi wategemee kwamba miundombinu inakuwa rafiki," alisema Kasekenya.

Aliongeza kuwa makandarasi wakishirikiana na trafiki wahakikishe pia wakati ujenzi ukiendelea alama za barabarani ziwe ni za kueleweka kwa watumiaji, zenye kuonyesha nani apite wapi na kwa wakati gani.

Aidha, alisisitiza kuwa barabara zote zinazojengwa kuzingatia ubora wa viwango vya kimataifa, makandarasi wazingatie maeneo yote ambayo maji yalikuwa yanajaa mvua zikinyesha wahakikishe changamoto hiyo haijitokezi tena.

"Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADs) mkasimamie hilo, kabla makandarasi hawajatoka 'site' tuhakikishe kwamba hilo tatizo limeondolewa, hatutegemei tupate tena hiyo adha ambayo imekuwa ikiwakumba wakazi wengi wanaotumia barabara za Dar es Salaam. Changamoto kubwa sana ni miundombinu ya kutoa maji barabarani.

"Mvua zikinyesha maji yanajaa, hili mlichukulie kwa uzito unaostahili. Pia kuna wananchi wanalalamika baada ya ujenzi kuanza wanapata maji mengi kutoka barabarani na kusababisha mafuriko, tumeonyeshwa dizaini za mifereji ambayo itawekwa hivyo hatutegemei mvua zikinyesha kuona maji yanajaa kwenye nyumba za watu," alisema Kasekenya.

Hata hivyo, alisema wanamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha miundombinu inakuwa vizuri, na kwamba katika miradi hiyo hawajapata changamoto yoyote kutoka kwa makandarasi kwenye suala la malipo ya mradi huo unaoendelea ambayo kwa awamu ya tatu umefikia asilimia 53.

Vile vile, alitoa rai kwa wananchi kutumia vizuri miundombinu hiyo na kuilinda inavyotakiwa, kwasababu itasaidia kupunguza muda wa kusafiri na kurahisisha usafiri.

**HABARI KITAIFA**

# TLS, LHRC zalaani madai binti kubakwa

**Na Jenifer Gilla**

TUKIO la kikatili la binti mkazi wa Yombo Dovya, Temeke, Dar es Salaam, ambaye hajajulikana umri wake, kubakwa na kulawitiwa na vijana watano kwa wakati mmoja wanaodaiwa kuwa askari, limewaibua wadau wa sheria na haki za binadamu.

Wadau hao ni pamoja na Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC).

Wamelitaka Jeshi la Polisi kuwakamata askari hao na bosi wao, huku Wakili Peter Madeleka akisema ndani ya saa 24 kama Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) atashindwa kuwapeleka mahakamani askari hao atatekeleza wajibu huo kwa gharama zake.

Aidha, baadhi ya wadau wameendelea kumtafuta binti huyo ili kumpa msaada wa kisheria na michango mbalimbali kwa ajili ya kumwezesha kimaisha kwa kile walichosema kwa sasa anahitaji msaada mkubwa kisaikolojia.

Tukio hilo liliibuliwa juzi na aliyekuwa Meya wa Ubungo, Boniface Jacob, kupitia ukurasa wake wa X huku akiwa- tag (nakala), Rais Samia Suluhu Hassan, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stergomena Tax na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dorothy Gwajima.

Alisema wakati vijana hao wanamfanyia ukatili binti huyo, walimpiga picha mjongeo na kuzisambaza kwenye mitandao ya kijamii, wakidaiwa kutumwa na bosi wao aliyedai kuwa binti huyo ana uhusiano wa kimapenzi na mumewe.

**KAULI YA LHRC**

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga (pichani), alisema wanakemea vikali tukio hilo na kuwasihi wananchi kutii amri ya Jeshi la Polisi kutosambaza video hiyo kwa kuwa ni mbaya na inazidi kumdhalilisha huyo binti na familia yake.

Alisema wakiwa sehemu ya jamii, wamehuzunishwa na ukatili huo na kusisitiza wahusika wakamatwe na kufikishwa mbele ya sheria, ili ichukue mkondo wake na kulinda heshima ya vyombo hivyo.

Pia aliviomba vyombo vyote vya ulinzi na usalama kuungana kuwatambua na kuwakamata wahusika na kama kweli ni wanajeshi, wachukulie hatua za kijeshi na kiraia kuhakikisha haki inatendeka ili kurudisha imani ya jamii kwa jeshi hilo.

"Jeshi letu la Tanzania ni jeshi lenye heshima barani Afrika na duniani lihakikishe linajitenga na kashfa hii ya ubakaji wa raia wake ambao lina jukumu la kuwalinda kama kweli wahusika ni wanajeshi," alisema.

Pia alimwomba Rais Samia kujitokeza hadharani na kukemea udhalilishaji na ukatili huo dhidi ya mtoto wa kike akiwa mzazi na kiongozi mwenye dhamana ya kulinda raia wa Tanzania.

Alisema kama vitendo hivyo vitafumbiwa macho hayo, mambo yatazidi kujitokeza zaidi katika jamii kwa mwavuli wa watu kutumia nafasi zao kuumiza na kudhalilisha wengine.

Alisema Ibara ya 12 ya Katiba ya Tanzania na Mkataba wa Kimataifa wa Kupinga aina Zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake wa 1979, vinalinda watu wa jinsia zote na kukemea ubaguzi wa aina yoyote.

"Vilevile Ibara ya 3 ya Mkataba wa Nyongeza wa Haki za Wanawake Afrika (Maputo) inazipa wajibu nchi wanachama kulinda heshima ya utu wa wanawake," alisema.

Dk. Henga alimpongeza Jacob kwa kutoa taarifa hizo kwenye mitandao ya kijamii, Jeshi la Polisi kwa kukemea kwa haraka na Waziri Dorothy kwa hatua za awali walizochukua.

**TAMKO TLS**

Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Boniface Mwabukusi, alisema chama hicho kinalaani kitendo hicho na kulitaka Jeshi la Polisi kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya wahusika.

Alisema TLS inatoa wito kwa jamii kuungana kupinga udhalilishaji, unyanyasaji na ukatili wa kijinsia wa aina yoyote ikiwamo kuacha mara moja kusambaza video zinazohusu tukio hilo ili kulinda haki ya mwathirika.

Naye Wakili Peter Madeleka kupitia ukurasa wake wa X aliandika: "Waliofanya 'ushetani' huo (aliweka picha) watakamatwa na utaratibu huu: Huyo mwanamke (aliyedhalilishwa) amtaje huyo mume wa afande aliyetembea naye.

"Mume wa afande akishajulikana tutamjua afande, baada ya hapo, afande atawataja hao 'mashetani' wenzake na halafu 'mashetani' wote wakamatwe."

Aidha, aliwaomba watetezi wa haki za binadamu kushirikiana na kutoa msaada wa dharura kwa binti huyo ukiwamo wa kimwili, kisaikolojia huku akiahidi kuchangia Sh. milioni mbili.

Alisema kosa la kusambaza video hizo limewarahisishia kazi mamlaka husika hivyo ni muhimu nguvu kubwa, ikaelekezwa katika kuwakamata kuwafikisha mahakamani waliotenda kosa hilo.

"Nataka nimhakikishie Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kama ndani ya saa 24 atashindwa kuwapeleka mahakamani hao 'mashetani', mimi Peter Madeleka nitafanya wajibu huo kwa fedha zangu," aliandika.

**ASKOFU MWAMAKULA**

Askofu Mkuu wa Kanisa la Uamsho la Moravian Tanzania, Emmaus Mwamakula, aliandika katika ukurasa wake wa Facebook kuwa kitendo alichofanyiwa binti huyo hakikubaliki na kutoa wito kwa serikali imchukue binti huyo na kumhifadhi kwa usalama wake.

"Akiwa mahali salama amtaje huyo mwanaume aliyetembea naye ili kumjua mke ambaye ndiye bosi aliyewatuma vijana waliomwingilia kinyume na maumbile na kumdhalilisha mbele ya kamera.

"Pia mamlaka ziueleze umma hatua zilizochukuliwa dhidi ya wahusika wote ambao ni huyo mke wa bosi na vijana aliowatuma. Haiwezekani jamii inakemea vitendo visivyo na maadili ikiwamo ikiwamo ulawiti halafu wenye dhamana ya uongozi wawalipe watu kwa makusudi kutekeleza vitendo hivyo," alisema.

Askofu Mwamakula aliyataka mashirika ya kutetea haki kuingilia kati mara moja huku akitaka binti huyo kulindwa na kuondolewa kwa ajili ya usalama wake, ikiwamo Jeshi la Polisi na mamlaka nyingine kutoishia kulaani kitendo hicho bali umma ujulishwe kupitia wizara ni hatua gani zilizochukuliwa tangu kuvuja kwa video hiyo.



## Serikali yaondoa hofu, hakuna mgonjwa wa Mpox nchini

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Afya imesema kuwa nchi ni salama na hakuna mgonjwa wa homa ya nyani ambayo inasababishwa na virusi vya Mpox , huku ikitangaza hatua za kujikinga kwa kila mwananchi.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma, iliyotolewa jana na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Englibert Kayombo, kuanzia Mei 2022 ugonjwa huo ulipoanza hadi kufikia Mei 2024 wagonjwa 97,745 na vifo 203 vimetokea katika nchi 116 duniani.

Alisema ugonjwa huo unaweza kusambaa kutoka kwa mtu mwenye maambukizi kwenda kwa mwingine kwa njia za maji maji ya mwili ikiwamo mate, maharishi, jasho, mkojo na matone ya mfumo wa njia ya hewa.

Pia, ngozi kupitia kugusana na kujamiiana na mtu mwenye maambukizi ama kutumia vifaa, matandiko au kugusa sehemu zilizo na vimelea vya ugonjwa huo.

Alisema ugonjwa huo unaweza kuenezwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu.

"Dalili kuu ya Mpox ni upele, malengelenge au vidonda kwenye mwili hasa mikononi na miguuni, kifuani, usoni na wakati mwingine sehemu za siri.

Nyingine ni homa, maumivu ya kichwa, misuli, mgongo, uchovu na kuvimba mitoki," ilisema taarifa hiyo.

Kayombo alisema ugonjwa huo haujaingia nchini hivyo ni vyema kushirikiana kuhakikisha nchi inabaki salama.

Wizara imewataka wananchi kupiga namba 199 bila malipo endapo wataona mtu mwenye dalili za ugonjwa huo, kuepuka kugusana majimaji ya mwili au ngozi.

Pia kuepuka kusalimiana kwa kupeana mikono, kukumbatiana na kubusiana na mtu mwenye dalili, kunawa mikono kila mara kwa maji yanayotiririka au kutumia vitakasa mikono.

Pia kuepuka kula au kugusa mizoga au wanyama mfano nyani au swala wa msituni, kuvaa barakoa iwapo itabidi na kuongea kwa karibu na mtu mwenye dalili za ugonjwa huo, kuwahi kituo cha afya waonapo dalili.

Alisema wizara imeiamuru ufuatiliaji wa wagonjwa hasa vituo vya afya mipakani na kuhakikisha vifaa tiba na kinga vipo maeneo ya kutolea huduma.

# Ajira mpya 37,616 kutangazwa

**Na Lusungu Helela,**
SUMBAWANGA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu, amesema serikali imepanga kutangaza ajira mpya 37,616.

Amesema ajira za kada ya ualimu, afya, uhasibu, ugavi na kada nyinginezo tayari zinaendelea kutangazwa, lengo likiwa ni kupunguza tatizo la upungufu wa watumishi nchini.

Alisema hayo jana kwa nyakati tofauti wakati akizungumza katika mikutano ya hadhara iliyofanyika katika vijiji vya Kitete, Laela, Kamsamba na Kavifuti vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, mkoani Rukwa, ikiwa ni ziara yake ya kwanza tangu alipouteliwa kushika wadhifa huo.

Akizungumzia nafasi za ajira za ualimu ambazo tayari zimeshatangazwa na Sekretarieti ya Ajira kwenye ngazi ya mikoa kulingana na mahitaji ya mkoa husika, Sangu alisema utaratibu wa kuwapata walimu kwa mwaka huu umeanza kuwa wa tofauti ukilinganisha na miaka ya nyuma.

Alisema kuwa usaili huo umeanza kufanyika kwa kada ya ualimu kwa sababu nafasi za ajira za ualimu ni chache ukilinganisha na idadi ya walimu wa shule ya msingi na sekondari waliohitimu vyuo mbalimbali hapa nchini, ambapo zaidi ya walimu 100,000 wapo mtaani hawana ajira.

Sangu alisema serikali imekuja na uamuzi huo ili kuchagiza dhana ya ushindani kwa lengo la kuhakikisha kila mwenye sifa stahiki anapata ajira katika mazingira aliyopo pasipo kulazimika kusafiri kwenda Dodoma au Dar es Salaam kwa ajili ya kufanya usaili.

Kufuatia hatua hiyo, Sangu alitoa wito kwa vijana waliohitimu vyuo mbalimbali hapa nchini kuchangamkia nafasi hizo za ajira, huku akiwataka wajiandae ipasavyo kwa ajili ya usaili huo, ikiwa ni mara ya kwanza kwa kada hiyo ya ualimu kufanya usaili.

Kadhalika, alitumia fursa hiyo kuwatoa wasiwasi waombaji wa nafasi hizo za ualimu, huku akiwahakikishia kuwa ofisi yake yenye dhamana ya kusimamia masuala ya ajira nchini imejizatiti kuhakikisha mchakato huo wa kuwapata walimu wenye sifa stahiki utakuwa wa huru na haki.

Alisema: "Katika kumsaidia Waziri wangu (George Simbachawene) tutahakikisha Sera ya Ajira nchini inayosisitiza haki ya kupata ajira bila kujali hali ya kiuchumi, rangi, kabila na dini inazingatiwa kikamilifu."

# Uingereza kuisaidia Tanzania mapambano ugonjwa UKIMWI

**Na Mwandishi Wetu**

BALOZI wa Uingereza nchini, David Concar, amesema nchi yake itaendelea kuiunga mkono serikali katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI ili kutimiza malengo ya kutokomeza maambukizi mapya, unyanyapaa na vifo vinavyohusiana na Virusi Vya Ukimwi (VVU).

Alisema hayo wakati wa mapokezi ya wapanda mlima Kilimanjaro 71 waliokuwa wakishiriki kampeni ya kila mwaka ya GGM Kili Challenge mjini Moshi, Kilimanjaro.

Kampeni hiyo imeandaliwa na kampuni ya dhahabu ya Geita Gold Mining kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Kupambana na UKIMWI (TACAIDS).

"Njia kuu ambayo Uingereza inafanya ni kuwa mmoja wa wachangiaji wakubwa wa mfuko wa kimataifa wa kupambana na UKIMWI, kifua kikuu na malaria, kwa miaka mitatu kutoka 2024 hadi 2026. Uingereza itatoa Pauni bilioni moja kwa mfuko huo, ambao kwa jumla utatoa Dola milioni 602 kwa Tanzania," alisema.

Mwakilishi kutoka Geita Gold Mining, Nzuamkende alisema kampeni hiyo inayofanyika kwa mwaka wa 22, inalenga kukusanya fedha na kuichangia serikali ili kufikia malengo ya sifuri tatu.

Aidha, aliwashukuru wafadhili na washiriki kutokana na michango wanayoitoa kufanikisha kampeni hiyo.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Dk. Jerome Kamwela, alisema Tanzania inafanya vizuri kuelekea malengo ya kimataifa ya muda mrefu na ya kati ambayo ni kufikia 95 tatu ifikapo mwaka 2025.

Alisema tawimu zinavyoonesha kuwa kuna watu milioni 1.7 wanaishi na VVU, hivyo 95 ya kwanza ni kuona watu hao wanatambuliwa na kujua hali zao ambapo sasa imefika asilimia 83.

Alisema 95 ya pili ni wale wanaoishi na VVU watumie dawa za kufubaza makali ya UKIMWI kwamba Tanzania imevuka lengo kwa kufikisha asilimia 98 na 95.

Alisema 95 ya tatu ni wale wanaotumia ARV wawe wamefubaza virusi, utafiti wa mwisho unaonyesha maambukizi mapya yakipungua.




## TAMISEMI yapata dawa vitendo vya ukatili kwa wanafunzi

**Na Agustino Kihombo,** IRINGA

KATIKA kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi, utoro na ukosefu wa chakula shuleni, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imeanzisha mpango wa shule salama.

Mpango huo utasaidia kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi na kuwawezesha kufikia ndoto zao kielimu.

Akizungumza katika mafunzo ya wakufunzi wa mpango wa shule salama yaliyofanyika mkoani Iringa, mratibu wa mpango huo kitaifa, Hilda Mgomapayo, alisema utafiti umebaini kuwa, zipo changamoto zinazochangia wanafunzi wa shule za sekondari washindwe kumaliza mzunguko wao wa elimu na kuathiri ndoto zao.

Alisema miongoni mwa changamoto hizo zinasababishwa na wazazi, jamii na walimu.

"Mpango huu unalenga kubadilisha mitazamo, tabia na mwelekeo wa jamii kwa ujumla dhidi ya watoto ili tuweze kuwalinda na kuwaepusha na vitendo vya ukatili ili tuwawezeshe kukamilisha mzunguko wa elimu," alisema Mgomapayo.

Alisema, lengo la serikali ni kupunguza vikwazo hivyo kwa wanafunzi na kufanya shule kuwa eneo salama kwa mtoto kufikia ndoto zake kupita mpango wa shule salama nchini. Mpango huu ni mpya na unaratibiwa na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, chini ya mradi wa kuboresha shule za sekondari (SEQIP).

"Baada ya mafunzo haya ya wawezeshaji wa kitaifa tunategemea wataenda kuwawezesha watekelezaji wa mpango huu katika ngazi za mikoa, wilaya hadi kata ambao watakuwa ni maofisa maendeleo ya jamii ngazi ya kata ambako ndiko jamii iliko, watafanya ulaghibishi na uchechemuzi na mafunzo kwa jamii," alisema.


Kwa upande wao baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo akiwamo, Reginaldo Msendekwa na Saida Mgeni walisema mpango wa shule salama umekuja wakati mwafaka ambapo wanafunzi wanakabiliwa na vitendo vya ukatili wa kijinsia kuanzia nyumbani hadi shuleni.

Alisema: "Kimsingi shule salama ni jumla ya mahitaji yote anayoweza kuyapata mwanafunzi ikiwamo chakula, malazi, vitendea kazi pamoja na uwepo wa mazingira mazuri ya kujifunzia, haya yote yanaweza kumfanya mtoto kuwa salama na kufanikiwa kufikia ndoto zake kwani anapoyakosa hulazimika kuyatafuta nje ya utaratibu na ndiyo maana wengi wanafanyiwa ukatili."

Pamoja na mambo mengine ya kuboresha elimu mpango huo pia utasaidia kuimarisha utoaji wa chakula shuleni na kuzingatia miundombinu ya mahitaji maalumu.

TANGAZO

yapı merkezi






**Hongera, Tanzania!**

***Yapi Merkezi - Tunajenga Mustakabali Bora Pamoja***

Yapi Merkezi tunayo furaha kusherehekea kukamilika kwa mradi wa Reli ya Kiwango cha Kimataifa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma.

Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Shirika la Reli Tanzania (TRC), wizara zote, watoa huduma, wakandarasi, benki na taasisi zinazotoa huduma za bima zilizoshirikiana nasi, wafanyakazi wa Yapi Merkezi, wadau wote wa mradi na wananchi wa Tanzania. Kujitoa na msaada wao kumekuwa muhimu katika kufanikisha mradi huu.

Yapi Merkezi imefanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha mafanikio ya mradi huu. Licha ya changamoto zote, tulitimiza ahadi yetu na tumeheshimika kuwa sehemu ya kutimiza ndoto ya kukamilika kwa mradi huu. Wakati Watanzania wakifurahia SGR na manufaa yake makubwa kwa nchi, tutaendelea kusaidia sekta ya reli ya Tanzania huku tukisonga mbele pamoja.

**Tuliahidi, Tumetimiza.**
**Hongera Tanzania, Hongera Mama Samia,**
**#KAZI IENDELEE**

**www.ym.com.tr**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Nishati safi itumike kupunguza uchafuzi wa hewa

**KUNA** umuhimu wa kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya gesi ili kuepuka uchafuzi wa hewa ambao unasababisha uharibifu wa mazingira na pia kusababisha magonjwa mbalimbali.

Matumizi ya kuni na mkaa huchangia uharibifu wa hali ya hewa.

Moshi unaovutwa kutoka kwenye kuni na mkaa husababisha athari kubwa ya magonjwa yanayosababishwa na hewa chafu.

Ulinzi wa afya ya mama, familia, mazingira na taifa dhidi ya mabadiliko ya tabianchi ni lazima uanzie jikoni.

Mkutano Mkuu wa Maboresho ya Serikali za Mitaa (TOA), ulieleza kuhusu nia ya serikali ya kufikia asilimia 80 ya Watanzania wote kutumia nishati safi ifikapo mwaka 2034.

Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa kinara wa kutangaza matumizi ya nishati safi ya kupikia na lazima taifa lianze sasa kubadilisha nishati inayotumika kupikia.

Mara kwa mara anapokuwa kwenye majukwaa mbalimbali ya matumizi ya nishati safi ya kupikia, Rais anasema huwezi kumaliza au kupunguza ukataji miti unaoangamiza misitu kama hutaligusa jiko.

Kampeni ya Rais imefanya mengi, Watanzania wameelezwa umuhimu wa matumizi ya teknolojia za kupikia zinazopunguza madhara kiafya, athari kwa mazingira na kijamii.

Na sasa Rais amelifikisha taifa kwenye kutekeleza Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia 2024 - 2034.

Analenga kaya zenye 'jiko safi na salama', ambayo asilimia 80 ya Watanzania watakuwa wanatumia jiko lenye nishati safi ya kupikia ifikapo 2034.

Pamoja na kuwaondoa kinamama katika matumizi ya kuni na mkaa na kutumia nishati safi, pia taasisi kubwa ambazo zinahudumia watu wengi kupata chakula, zinahimizwa kuhama kwenye matumizi ya kuni na mkaa na kuhamia kwenye nishati safi ili kupunguza uharibifu wa hewa na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Hata hivyo, ili kufanikiwa katika matumizi ya nishati safi ipo haja ya kuwa uhamasishaji wa kutumia majiko yanayotumia nishati safi na yapatikane kwa urahisi ili wanayoyahitaji wasipate vikwazo kuyapata.

Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS) inaeleza kuwa Tanzania Bara ina takribani kaya milioni 13.9.

Kufikia azma hiyo kaya zenye jiko safi na wakuu wa mikoa na wilaya wasimamie matumizi ya nishati safi ya kupikia na pia wizara na taasisi za umma kadhalika na sekta binafsi kuzingatia matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kulinda mazingira na kuepusha athari nyingi zinazotokana na kutumia nishati zisizo safi.

Mwaka jana Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira iliagiza taasisi zote zinazohudumia watu zaidi ya 100, ifikapo Januari, mwaka huu, ziache kutumia kuni na mkaa kupikia.

Ofisi ya Makamu wa Rais, katika mikakati yake inaeleza kuwa hilo limefanyika na taasisi nyingi zikiwamo za umma kuanzia Magereza, kambi za jeshi, shule za sekondari, vyuo vya ualimu na vikuu vimeanza kutumia nishati safi ya kupikia.

Pia, juhudi zinafanywa na kila taasisi inayohusika na nishati na katika mbio za Mwenge wa Uhuru, mwaka huu, ujumbe mkubwa unaobebwa ni uhamasishaji wa matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Uhamasishaji huo utasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza matumizi ya kuni na mkaa na kuepusha athari zinazosababishwa na hewa chafu inayotokana na kuvuta moshi mchafu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Inapendeza HESLB mnavyojiongeza

Na Dk. Reubeni Lumbagala

**MABORESHO** katika sekta ya elimu kuanzia msingi, sekondari hadi vyuo vikuu yamechangia ongezeko kubwa la wahitimu.

Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia huku serikali ikibeba mzigo wa kutoa ruzuku ya elimu ya msingi bila ada kuanzia darasa ya awali hadi kidato cha sita ili watoto wasome bila vikwazo ni jambo la kujivuniwa.

Na pale wanafunzi hao wanapofanya vyema katika mitihani ya kidato cha sita na hatimaye kuendelea na masomo ya shahada katika vyuo vikuu, serikali imekuwa ikitoa mikopo kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Haya yote yanafanyika kwa nia njema ya kuhakikisha vijana wa Tanzania wanakuwa na maarifa, ujuzi na stadi stahiki za kuwawezesha kujitegemea.

Moja ya changamoto katika mfumo wetu wa elimu kabla ya maboresho ya mitaala yaliyofanyika ilikuwa ni ukosefu wa ujuzi wa kuwezesha vijana kuajiriwa au kujiajiri wenyewe baada ya elimu zao na wengine hata baada ya kozi.

Ni wazi wahitimu wa kada mbalimbali wamekuwa wakiandaliwa kuajiriwa bila kuwa na stadi na ujuzi wa kujiajiri, hali hii ikapelekea serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kuchukua hatua.

Mikakati ya kuziba udhaifu huu ni pamoja na kufanya maboresho ya mitaala ambapo sasa mafunzo ya amali yanapewa msukumo mkubwa ili kuwajengea uwezo wanafunzi kuwa na ujuzi wa kuwasaidia kujitegemea bila kutegemea ajira rasmi.

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), inachochea maendeleo ya elimu kwa kutoa mikopo, lakini kuwasaidia wanufaika kuwa na ujuzi stahiki ambao utakuwa nyenzo muhimu ya kuajiriwa na kujiajiri na hatimaye kuwa na uwezo wa kurejesha mikopo waliyokopeshwa.

Ni katika muktadha wa kuwajengea uwezo wahitimu ili kuajiriwa kirahisi au kujiajiri, bodi imeandaa mafunzo rasmi ya kuwasaidia wahitimu ili wawe na ujuzi ambao ni mtaji muhimu katika maisha yao, hasa baada ya kuhitimu masomo yao.

Bodi kwa kushirikiana na Taasisi ya Adanian Labs wameandaa mafunzo kwa wanafunzi wa mwaka wa mwisho na wahitimu katika michepuo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHEMA) na Sayansi ya Kompyuta ili kuwawezesha kujiajiri au kuajiriwa, na hivyo kuwa na vipato ambavyo pamoja na kuendesha maisha yao, watachangia maendeleo ya uchumi wa nchi. Vilevile, watakuwa na uwezo wa kurejesha fedha walizokopeshwa wakiwa vyuoni.

Hivyo basi, mbali na kutoa mikopo na kuwadai wanufaika wake, sasa imeamua kujiongeza na kufanya jitihada za kuwatafutia fursa wanufaika wake ili wawe na uwezo wa kurejesha fedha na hatimaye wengine waweze kusoma kupitia marejesho ya fedha zao. Hii ni hatua murua na ya kupongeza sana.

Mafunzo haya muhimu yenye lengo la kuwajengea uwezo wanafunzi wa mwaka wa mwisho na wahitimu wa fani za TEHAMA na kompyuta ambao ni wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu yatasaidia sana kuwaongezea umahiri, stadi na ujuzi ambao ni muhimu sana katika kujitegemea kiuchumi badala ya kubaki nyumbani wakisubiri ajira rasmi kutoka serikalini au katika sekta binafsi.

Ikumbukwe kuwa, mafunzo haya yatatolewa bure kwa njia ya mtandao kwa kipindi cha miezi minne kuanzia wiki hii Agosti 5, 2024. Kwa kuwa, mafunzo haya yataendeshwa kwa njia ya mtandao, kila mwombaji anapaswa kuwa na kompyuta na intaneti ili kuweza kujifunza kikamilifu na kupata ujuzi na stadi muhimu.

Wahitaji wajue kuwa, kwa zama hizi za ushindani katika soko la ajira, mhitimu mwenye ujuzi wa kutosha anajiweka katika nafasi nzuri ya kuajiriwa na kujiajiri na ndiyo maana taasisi mbalimbali zinashauriwa kutoa fursa kwa wahitimu kujitolea katika taasisi zao ili kuwaongezea ujuzi wanafunzi na wahitimu kwani ujuzi huo ni muhimu katika kujitegemea kiuchumi.

Sanjari na hilo, uamuzi wa HESLB kushirikisha wadau wengine kuwajengea uwezo wanafunzi na wahitimu ni wa kupongezwa kwani unasaidia moja kwa moja kupunguza tatizo la ajira kwa vijana wa Tanzania kwa kuhakikisha wanapata ujuzi na stadi zinazoendana na; mazingira na ushindani wa soko la ajira. Kwa wataalamu wa TEHAMA na kompyuta jitokezeni kwani fursa hii si ya kuichezea, ombeni kujiunga na mafunzo haya ili mjiongezee uwezo na ujuzi na hatimaye muwe na uwezo wa kujitegemea kiuchumi na kulipa fedha mlizokopeshwa mkiwa vyuoni kwa maendeleo ya nchi yetu.

## Bandari haihusiki 'tozo ya udongo' Kigoma

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Bandari Tanzania (TPA), imesema haihusiki na makusanyo ya malipo ya usafirishaji wa abiria na mizigo Bandari za Kigoma ambazo zimelalamikiwa hivi karibuni.

Meneja wa Bandari za Ziwa Tanganyika, Edward Mabula, amesema tozo maalumu inayotozwa kwa wageni wanaoingia Tanzania hutozwa na taasisi nyingine.

Uchunguzi umebaini malipo yanayofahamika kama "Kodi ya Udongo" hukusanywa na Wakala wa Meli (Shipping Agencies) na kuwasilishwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mujibu wa sheria.

Mawakala wa meli ni kampuni binafsi zinazofanya biashara ya uwakala wa meli nchini kwa mujibu wa sheria, pamoja na gazeti hili kujulishwa kuwapo malalamiko ya baadhi ya watu wachache wasio waadilifu wanaoweza kufanya wizi.

Juzi zilitolewa taarifa za ufujaji wa mapato bandarini chanzo cha taarifa kikiwa ni maoni ya wadau wa Sekta ya Biashara yaliyotolewa katika Kikao cha Baraza la Biashara la Mkoa wa Kigoma kilichoketi Agosti 31, 2024 na kuongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye.

Katika kikao hicho ambacho TPA ilishiriki kama mdau muhimu wa maendeleo ya sekta ya biashara, hoja mbalimbali zilitolewa na kujadiliwa kwa lengo la kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara ili kuongeza tija na ufanisi.

"TPA haitozi tozo iliyotajwa katika habari hiyo. Kimsingi, tozo iliyotajwa ni malipo yanayofahamika kama "Kodi ya Udongo" ambayo hutozwa na taasisi nyingine," alisema Mabula.

Mabula alisema TPA inaendelea kushirikiana na taasisi nyingine za Umma katika utoaji wa huduma za kibandari na ukusanyaji wa tozo na mapato ya serikali kwa mujibu wa sheria za nchi.

Alisema ni vyema maazimio ya kikao tajwa yakaendelea kufanyiwa kazi na wadau wa Sekta ya Biashara Mkoa wa Kigoma kwa kuzingatia kanuni na miongozo inayosimamia utendaji kazi wa mabaraza husika.

Alisema ni vyema wadau muhimu kutojihusisha na upotoshaji wa makusudi unaofanywa na baadhi ya watu wenye nia ovu ya kuchafua sifa nzuri ya mamlaka na kufifisha juhudi kubwa zinazofanywa na serikali kuimarisha uchumi kupitia shughuli za sekta ndogo ya Bandari.

"TPA haina tozo ya Dola za Kimarekani 10 wala Dola tano, malalamiko ya Dola 25 hadi 30 yanaashiria kuwa mteja wa aina hiyo anakuwa amekutwa na ukiukwaji wa taratibu za sheria na hivyo hulipa kama hongo ili kuepuka adhabu na huo sio utaratibu," alifafanua.

Mabula alisema malipo yote hutolewa risiti halali na iwapo kuna yanayofanyika bila risiti halali, mteja anasisitizwa kutoa taarifa katika mamlaka husika kwa hatua za kisheria.

"Hakuna upotevu wowote wa mapato unaotokea katika Bandari za Kigoma, tozo na makusanyo yoyote yapo kisheria na yamekuwa yakifanywa kwa kuzingatia sheria na taratibu za bandari," alisema Mabula.

Katika kikao hicho, Mwenyekiti wa Baraza ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye, alizielekeza taasisi zinazohusika kuangalia uwezekano wa kuhuisha mifumo na taratibu zao ili ikiwezekana tozo zote zikusanywe sehemu moja.



Sehemu ya wananchi wa Kata ya Lusaka, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga mkoani Rukwa wakimsikiliza Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu, baada ya kuwasili katika Kata ya Lusaka, ikiwa ni ziara yake ya kwanza tangu alipoteuliwa kushika wadhifa huo. **PICHA: LUSUNGU HELELA**

# NEMC na mikakati kutumia taka kama fursa kiuchumi

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na halmashauri nchini zimepanga kuja na mkakati wa kuzichakata taka ngumu na kuzigeuza kuwa fursa za kiuchumi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Immaculate Semesi, wakati wa kufungua mkutano ulioandaliwa na Kituo cha Sayansi na Mazingira cha India (CSE).

Mkutano huo uliwashirikisha maofisa wa halmashauri mbalimbali nchini wakiwamo maofisa wa Ofisi ya Rais Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa kwa lengo la kujadili namna ya kuzifanya taka kuwa fursa za kiuchumi.

Dk. Semesi alisema lengo kuu la mkutano huo ni kujadili namna ya kurejeleza taka ngumu hapa nchini na wamepanga kuanza mradi wa kurejeleza taka kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

Alisema tathmini iliyofanywa na CSE inaonesha kuwa nchi za Afrika bado ziko nyuma kwenye usimamizi, uhifadhi, usafirishaji na urejelezaji wa taka ngumu.

Alisema ni wakati mwafaka kwa halmashauri za manispaa kuunganisha teknolojia ya kidijitali katika programu za usimamizi wa taka ngumu ili kutengeneza taarifa za msingi ambazo zinaweza kutumika katika afua za kimkakati.

Alisema teknolojia hizo za kidijitali zitasaidia kupima utendaji kazi na mipango sahihi ya udhibiti wa taka katika miji mbalimbali nchini.

Alisema ili kudhibiti taka za kwenye Manispaa kuna haja kwa viongozi kuwa na mipango ya kuwa na takwimu na kuwekeza katika mifumo ya usimamizi wa taka.

Alisema pia wanahitaji kuimarisha teknolojia za kisasa, kuongeza uelewa wa umma katika masuala ya kiufundi na rasilimali watu, uwezo wa kifedha, kusimamia ipasavyo taka za manispaa na kutekeleza kanuni na miongozo ya manispaa.

Alban Mugyabuso ambaye ni Ofisa Usafirishaji Manispaa ya Kinondoni alisema lengo la mkutano huo ni kuzigeuza taka ngumu kuwa fursa za kiuchumi kwa vijana.

"Tumezoea taka zinakusanywa zinapelekwa dampo Pugu Kinyamwezi, lakini lengo hapa tunaelezwa namna ya kuzirejeleza kwa kutenganisha taka hatarishi na taka ngumu ili tuchukue taka ambazo haziozi zikafanye kazi zingine," alisema.

Alisema asilimia 65 mpaka 70 ya taka zinazozalishwa ni za kuoza hivyo zinaweza kuchukuliwa kutengeneza mbolea na gesi wakati chupa ngumu zitatumika kutengeneza bidhaa zingine za thamani wakati taka hatarishi ambazo haziwezi kurejelezwa kama pampasi ndizo zitapelekwa dampo.

"Kwa hiyo hapo tutakuwa tumesaidia mazingira kwasababu taka zinazooza zinazalisha hewa ukaa na hewa ukaa inakwenda kuharibu mazingira na kusababisha mabadiliko ya tabianchi na tutapunguza kwa kiwango kikubwa hewa ukaa na pia tutakuwa tumezalisha ajira kwa vijana," alisema.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



HABARI KITAIFA

# Waziri apiga marufuku walengwa mpango TASAF kufanyishwa kazi

**Na Lusungu Helela**

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu, amepiga marufuku walengwa wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kufanya kazi za kujitolea.

Walengwa hao ni wazee wenye umri wa zaidi ya miaka 65, wenye ulemavu, wajawazito na watoto, pia ameonya watendaji watakaozembea kusimamia suala hilo watachukuliwa hatua kali za kinidhamu dhidi yao.

Sangu ambaye ni Mbunge wa Kwela alisema hayo jana kwa nyakati tofauti wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Lusaka kwenye mikutano ya hadhara iliyofanyika kwenye vijiji vya Lowe, Lusaka, Kizumbi na Kamnyazya, wilayani Sumbawanga mkoani Rukwa.

Alizitaja kazi hizo za kujitolea ambazo huratibiwa na TASAF kuwa ni ulimaji wa barabara na uchimbuaji wa mitalo ya barabara. Alisema makundi hayo yasisumbuliwe kufanya kazi hizo kwa kuwa si sawa kutokana na hali zao.

Sangu pia alizitaka kaya zinazonufaika na mpango wa TASAF kuhakikisha kama zina wanafunzi waliohitimu kidato cha sita na wanatarajia kujiunga na vyuo vikuu, ziwasilishe majina katika ofisi za halmashauri zao ili kupata kipaumbele cha kupata mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kwa kuwa bodi hiyo imeingia mkataba na TASAF.

Alisema lengo la TASAF kuingia mkataba na HESLB ni kuhakikisha watoto wanaotoka katika kaya maskini hawakosi mkopo ili wafaulu na baadaye kurudi kwa ajili ya kuzikomboa kaya zao kwenye lindi la umaskini.

Sangu alisema ni jambo lisilokubalika chini ya serikali ya sasa kuona mtoto aliyetoka kwenye kaya maskini amesoma na wazazi wake ni wanufaika wa TASAF lakini anakosa mkopo anapotaka kujiunga na elimu ya chuo kikuu.

Kutokana na hali hiyo, Sangu aliwaagiza waratibu wa TASAF wa mikoa na wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kuhakikisha wanawasaidia watoto hao ili kutimiza ndoto zao.

Pia alizitaka kaya zenye watoto ambao ni walengwa wa TASAF lakini hawajabahatika kujiunga kidato cha kwanza, wachangamkie fursa ya ufadhili wa masomo unaotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu kujiunga na VETA



Mwonekano wa Daraja la Ruaha Mkuu lenye urefu wa mita 133 pamoja na barabara ya Kidatu –Ifakara yenye urefu wa kilomita 66.9 iliyokamilika kujengwa kwa kiwango cha lami ambayo imefunguliwa rasmi na Rais Samia Suluhu Hassan mkoani Morogoro juzi. **PICHA: WIZARA YA UJENZI**

# Nchimbi: Ahadi ya Rais Samia Kigoma kuwa lango kuu kibiashara yatekelezwa

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, amesema ahadi ya kuufungua Mkoa wa Kigoma kuwa lango kuu la biashara inaendelea kutekelezwa kwa vitendo.

Balozi Nchimbi amesema ahadi hiyo ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, inatekelezwa kwa hatua thabiti, kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo inalenga kuzidi kuufungua mkoa huo, kuendelea kuunganisha na mikoa mingine na kuiunganisha Tanzania kibiashara na nchi zingine kupitia Kigoma.

Alisema hayo juzi wakati akihutubia maelfu ya wananchi wa Kigoma, katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Uwanja wa Mwanga Community Centre, mjini Kigoma jana.

Alizitaja hatua zinazochukuliwa na serikali, kuwa ni pamoja na ujenzi wa barabara za lami, ujenzi wa meli mbili kubwa kwa ajili ya kuboresha usafiri wa Ziwa Tanganyika, ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Kigoma na kutoka Kigoma kwenda nchi za jirani pia mipango ya kuiboresha Reli ya Kati.

"Nimeambiwa ahadi mbalimbali ambazo Mheshimiwa Rais Samia alitoa, ikiwamo ya kuufungua Mkoa wa Kigoma. Ninyi ni mashahidi kuwa ahadi hiyo imeendelea kutekelezwa kwa vitendo. Mchakato wa barabara za lami unaendelea Kasulu, Kibondo na Buhigwe.

"Lakini juzi mmesikia wakati Rais anazindua treni ile inayotumia umeme (SGR), kuwa dhamira ni kuifikisha Kigoma. Pia mchakato wa kuiboresha Reli ya Kati unaendelea. Hebu pigeni picha kubwa yote haya yakikamilika, Kigoma itafunguka haijafunguka," alisema Balozi Nchimbi.

Pia, alielekeza utekelezwaji wa ahadi ya kuipatia Mkoa wa Kigoma umeme wa uhakika kwa kuunganisha kwenye gridi ya taifa, ifikapo mwezi Machi, 2025, ambapo ujenzi wa vituo vya kupozea umeme katika maeneo ya Nguruka na Kidahwe uko katika hatua za mwisho kukamilika.

Katika ziara hiyo ikiwa ni siku ya kwanza mkoani humo, Balozi Nchimbi, alipokea mamia ya wanachama wapya waliojiunga CCM kutoka vyama vingine, wakiongozwa na aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Kigoma, Sabrina Sungura na Diwani wa Kata ya Mwakizega, Wilaya ya Uvinza, Patrick Bitaliho kutoka Chama cha DP.

Hatua hiyo ni mwendelezo wa chama hicho kupokea wanachama na viongozi wa vyama vya upinzani kujiunga CCM kupitia ziara hizo za Katibu Mkuu CCM zinazofanyika katika mikoa mbalimbali.

# Naibu Waziri ahimiza elimu biashara kaboni

**Na Gwamaka Alipipi**

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI (Afya), Dk. Festo Dugange (pichani chini), amekishauri Kituo cha Taifa cha Ufuatiliaji na Usimamizi wa Biashara ya Kaboni (NCMC), kupanua wigo wa utoaji wa elimu kuhusu fursa na manufaa ya biashara hiyo kwa wananchi.

Alitoa agizo hilo juzi alipotembelea banda la Ofisi ya Makamu wa Rais katika maonesho ya Sikukuu ya Wakulima Duniani (Nanenane), yanayofanyika kitaifa katika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma.

Alisema iwapo elimu ya kutosha kuhusu biashara ya kaboni itatolewa kwa wananchi, hususani kupitia fursa ya upandaji miti itasaidia uelewa kuhusu uhifadhi wa mazingira na kuongeza kipato katika ngazi ya kaya na jamii kwa ujumla.

Dk. Dugange alisema zipo baadhi ya mamlaka za serikali za mitaa zinazotekeleza miradi ya biashara ya kaboni na hivyo kutoa ushauri kwa NCMC kubuni na kuweka mipango mahususi ya kushirikiana na halmashauri hizo katika utoaji wa elimu.

"Kituo cha Taifa cha Ufuatiliaji wa Kaboni hakina budi kujitangaza ili kiweze kufahamika na kufikia wadau wengi ikiwezekana hata kufungua ofisi za kanda katika mikoa mbalimbali nchini". Alisema Dk. Dugange.

Alisema ni wakati mwafaka kwa serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha elimu ya biashara ya kaboni inatolewa, akisema bado jamii haina uelewa wa kutosha kuhusu kaboni pamoja na fursa na faida zilizopo katika biashara hiyo.

Kadhalika, aliitaka Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia NCMC kufanya mikutano na makongamano na wadau ili kutoa elimu kwa wananchi na taasisi mbalimbali za uwekezaji ambao ndio walengwa wakubwa wa biashara ya kaboni nchini.

Pia, alisisitiza kuwapo kwa wataalamu wengi ambao watasaidia katika kutoa elimu hiyo, akisema kwa sasa inaonekana bado kuna uhaba wa wataalamu kwenye eneo hilo lakini jitihada ikiongezeka matunda yake yataonekana kwa kila mmoja.

Aidha, Dugange alizitaka halmashauri zote nchini kutenga bajeti kwa ajili ya masuala ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira na kuhakikisha miti yote inayopandwa inatunzwa na kustawi.





# Tani 61,000 za mbolea ya ruzuku zasambazwa Kanda ya Kaskazini

**Na Allan Isack,**
ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, amesema katika kipindi cha mwaka wa 2023/2024 serikali imetoa mbolea ya ruzuku tani 61,400 kwa wakulima katika mikoa mitatu ya Kanda ya Kaskazini.

Amesema mbolea hiyo imetolewa katika mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro yenye thamani ya Sh.bilioni 85.9.6, lengo likiwa ni kuboresha sekta ya kilimo.

Aliyasema hayo juzi wakati akifungua maonesho ya Nanenane Kanda ya Kaskazini, yanayoendelea viwanja vya Themi mkoani-Njiro Arusha.

Babu alisema serikali imeboresha miundombinu ya maji ili kupunguza utegemezi wa mvua katika kukuza mazao, imejenga na kukarabati mifereji na mabwawa yenye thamani ya Sh.bilioni 62.4.

"Mifereji hii iliyojengwa kwa Mkoa wa Manyara imegharimu Sh. bilioni 15.6, Mkoa wa Arusha (Sh. bilioni 38.4) na Kilimanjaro Sh.bilioni 8.4," alisema.

Alisema serikali imetoa mbegu za uhimilishaji za ruzuku kwa lengo la kuboresha aina za mifugo ambapo jumla ya ng'ombe 44,970 wamehimilishwa kwa mbegu bora za kisasa.

Pia, alisema lengo la serikali ni kuona wafugaji na kila Mtanzania mwenye uwezo wa kufanya kazi anafanya kazi wakiwamo wakulima na wafugaji nchini.

Aidha, alisema kumeanzishwa mashamba darasa ya malisho 12 kwa mikoa hiyo, lengo likiwa ni kutoa elimu ya ufugaji na uzalishaji wa malisho bora yenye thamani ya Sh.milioni 40.8 kwenye maeneo ya wafugaji.

Alisema serikali imeanzisha majosho, usambazaji wa dawa za kuogeshea mifugo na ugawaji wa vitendea kazi ikiwamo pikipiki kwa maofisa ugani.

Kadhalika, aliwaagiza wakuu wa wilaya za mikoa hiyo, kuimarisha ushirika kwa kuwa ndiyo utawakomboa kiuchumi wakulima.

Alisema sekta ya kilimo na uvuvi zimekuwa zikitoa mchango mkubwa katika kuongeza pato la taifa na mwananchi mmoja mmoja.

Alisema kuwa zaidi ya asilimia 90 ya wananchi wa kanda hiyo wanajihusisha na shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi.

Mwenyekiti wa Kamati ya maonyesho hayo, ambaye ni Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Missaile Musa, alisema washiriki ni kutoka taasisi na mashirika ya umma, kampuni na watu binafsi.




Balozi wa Uingereza nchini Tanzania, David Concar, akihutubia katika hafla ya kuwapokea wapanda Mlima Kilimanjaro waliokuwa wakishiriki kampeni ya kila mwaka ya GGM Kili Challenge yenye lengo la kusaidia miradi inayojikita katika kutokomeza VVU na Ukimwi. Kampeni hiyo imendaliwa na Kampuni ya Dhahabu ya Geita Gold Mining kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), jumla ya wapandamlima 48 na waendesha baiskeli 23 walishiriki zoezi hilo lilioanza Julai 19 kufikia tamati yake mjini humo hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Walimu msingi wapewa maagizo kuhusu chakula

**Na Hamida Kamchalla,**
TANGA

OFISA Elimu wa Jiji la Tanga, Shomari Bane, amewaagiza walimu wakuu wa shule za msingi kuweka mpango mkakati wa kuhakikisha wanafunzi wanakula chakula cha mchana shuleni.

Amesema ikiwezekana itungwe sheria ambayo itawabana wazazi na walezi watakaokaidi jambo hilo.

Aliyasema hayo juzi wakati wa vikao vya hamasa kuhusu ujenzi vilivyofanyika shule za msingi za Kange na Ziwani, kupitia Mradi wa Kuimarisha Ufundishaji na Ujifunzaji kwa Shule za Awali na Msingi (BOOST).

Alisema watoto wanapaswa kula chakula shuleni ili waweze kuwa na ufaulu mzuri wa masomo, hivyo amewataka wazazi na walezi kuchangia chakula na atakayekaidi kamati husika zimchukulie hatua.

Alisema: "Ili tuwe na wanafunzi bora katika masomo, ni lazima kila mtoto apate chakula na suala hili nitalifuatilia kwa ukaribu, walimu wakuu mnapaswa kuliweka kama sheria katika shule zenu," alisema Bane.

Alisema suala la elimu bila malipo bado watu wengi hawana uelewa wa hilo, kwa kuwa baadhi wanadhani serikali ndiyo inahusika kwa kila kitu na wazazi wengi kutokutaka kuchangia chakula kwa watoto wao.

"Ninataka wazazi mchangie chakula cha wanafunzi kwa kuwa msipofanya hivyo mtakuwa mnawatesa watoto wenu wenyewe ndio sababu nimetoa agizo hili kwa walimu kulisimamia," alisema.

Licha ya kuzungumza hayo, alisema wananchi wa eneo hilo wanapaswa kushiriki katika ujenzi kwa kujitolea nguvu zao ikiwamo kuchimba msingi wa vyumba vya madarasa.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kange, Aidan Munisi, alisema shule hiyo imepata Sh.milioni 88 na wananchi wameupokea mradi kwa mikono miwili na wako tayari kufanya kazi ambazo wameshirikishwa ikiwamo kujitokeza nguvu kazi zao.

Diwani wa Kata ya Maweni, Joseph Colyvas, alisema shule hiyo, ni ya zamani na imekuwa na majengo mengi chakavu.

Alisema utekelezaji wa mradi huo, utakwenda kuweka mazingira na madhari ya shule hiyo kuwa nzuri kwa kuwa wameupokea mradi na wako tayari kutekeleza.

## NEMC kutoa elimu ya mazingira kwa wakulima, wafugaji, wavuvi

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

BARAZA la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Kanda ya Kaskazini limejipanga kutoa elimu kwenye maeneo sita, ikiwamo utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwa wakulima, wafugaji na wavuvi.

Meneja wa NEMC Kanda hiyo, Benjamin Doto, akizungumza jana kwenye maonesho ya Nanenane Njiro jijini Arusha, alisema NEMC inatoa elimu kwenye maeneo sita ambayo ni ufanyaji wa Tathimini ya Athari kwa Mazingira (TAM), katazo la mifuko ya plastiki.

Pia namna ya kusajili miradi NEMC kwa kutumia mfumo kielektroniki (PMS), uchafuzi wa mazingira yatokanayo na kelele na kusikiliza kero na kutatua malalamiko yanayohusu masuala ya mazingira.

Hivyo, aliwataka wakulima, wafugaji na wavuvi kuzingatia matakwa ya Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 ikiwamo Tathmini ya Athari kwa Mazingira ili shughuli zao ziwe endelevu.

"Tunatoa elimu kwa umma na makundi yanayotembelea ni wakulima, wafugaji na wavuvi tunawasisitiza kuzingatia matakwa ya Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na kanuni zake hasa ufanyaji wa tathmini ya athari kwa mazingira na ukaguzi wa mazingira ya mwaka 2005, kanuni za kudhibiti kelele na mitetemo ya mwaka 2015," alisema.

Pia aliongeza: "Tunatoa elimu ya udhibiti wa taka ngumu hasahasa kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki hasa vifungashio ambavyo vinatumika kubebea bidhaa katazo lilishatolewa kisheria na kanuni zilitolewa mwaka 2019."

Alisema wananchi wamekuwa wakipewa elimu ya namna watakavyofanya shughuli zao kuwa endelevu na kuepuka kusababisha athari za mazingira.

Aidha, alitoa wito kwa wananchi kufika katika banda hilo ili kupata elimu ya mazingira na namna ya kufanya shughuli za maendeleo zinazohifadhi na kulinda mazingira.

## Kikongwe amwomba Majaliwa kumrudisha nyumbani


**Na Mary Mosha,**
MOSHI

MKAZI wa Kitongoji cha Hedaru wilayani Same mkoani Kilimanjaro, Maoud Matika (91) amemwomba Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa, amsaidie kumrudisha nyumbani kwao Mikindani mkoani Mtwara, kwa kuwa aliondoka huko tangu mwaka 1958.

Matika ambaye ni mlemavu wa macho na hali yake imedhoofika, akizungumza na Nipashe alisema katika harakati za kutafuta maisha alifika mkoani Kilimanjaro na kuanzisha makazi katika eneo la Ruvu wilayani Same.

"Nilikuja kufanya vibarua vya kulima katika maeneo ya Ruvu mwaka 1958 na nimeishi hapo hadi nilipopata ulemavu wa macho na ndipo nilipoanza kuomba," alisema.

Aidha, alisema watu pekee anaoweza kuwakumbuka ni mama yake mzazi, ambaye alifahamika kwa jina la Khadija na baadhi ya ndugu zake wakiwamo Issa, Said, Rashid na Matola.



## TFRA yaondoa mkanganyiko

**Na Renatha Msungu,** MWANZA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Kanda ya Ziwa imesema kazi yake ni kutoa elimu kwa wakulima nchini ili wawe na tija katika kilimo cha kisasa cha mazao ya chakula na biashara.

Kauli hiyo ya TFRA imelenga kuondoa mkanganyiko uliotanda miongoni mwa wakulima kuwa kazi yake si kuuza mbolea.

Akizungumza katika Maonesho ya Nanenane yanayofanyika katika viwanja vya Nyamhongolo mkoani hapa, Ofisa Udhibiti Mbolea wa TFRA Kanda ya Ziwa, Khanafi Mohamed, aliwataka wananchi kufika katika banda lao ili kupata elimu sahihi ya matumizi ya mbolea.

"Jambo hili tumekuwa tukilitolea elimu na kuwaonyesha sehemu sahihi ya kupata mbolea kwa ajili ya matumizi yao ya kilimo," alisema Mohamed na kusisitiza: "Sisi hatuuzi kabisa mbolea na katika hilo tunajitahidi kuwafikia wakulima wengi ili kuwapatia elimu zaidi."

Kwa upande mwingine, alisema mamlaka hiyo imejipanga kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea kwa wakulima wanaotembelea banda lao katika maonyesho hayo ili kuinua kilimo na kuongeza uzalishaji mazao ya chakula na biashara.

Meneja wa TFRA wa Kanda hiyo, Michael Sanga, alisema kumekuwapo na mwitikio mkubwa wa wakulima kutumia mbolea ya ruzuku baada ya kupatiwa elimu.

Sanya, alisema kama wadhibiti wa mbolea, watahakikisha elimu sahihi inamfikia kila mkulima katika kanda hiyo itasaidia kukabiliana na njaa na kuongeza kipato kwa wakulima kwani uzalishaji utaongezeka.

Alisema mamlaka hiyo imekuwa ikishirikiana na vyama vya ushirika katika kanda hiyo kusambaza mbolea ya ruzuku na maofisa ugavi kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea.

Maonesho hayo nchini kila mwaka kuanzia Agosti 1 hadi 8, hufunywa mahususi ya wakulima na wafugaji ili kujitangaza na kupata elimu kwa ajili ya kuboresha shughuli zao.

# Katibu AMCOS jela kwa uhujumu uchumi

**Na Alex Sayi,** MASWA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Simiyu imemhukumu aliyekuwa Katibu wa Chama cha Ushirika cha Msingi (AMCOS), wilayani hapa kutumikia kifungo cha miaka 15 jela kwa kosa la uhujumu uchumi.

Hukumu hiyo, ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Enos Misana, baada ya kumtia hatiani mshtakiwa huyo.

Akisoma hukumu dhidi ya mshtakiwa huyo, Hakimu Misana, alisema kuwa ushahidi uliotolewa kutoka upande wa Jamhuri, umeithibitishia mahakama hiyo bila kuwa na shaka yoyote kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo.

Alisema mahakama hiyo imetoa hukumu hiyo kwa mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa viongozi wengine wa vikundi vya kijamii wenye tabia kama hiyo.

Awali Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wa Wilaya ya Maswa, Bahati Madoshi Kulwa, alidai kuwa mshtakiwa huyo anakabiliwa na makosa mawili katika shtaka namba 1/2023 la uhujumu uchumi.

Madoshi alitaja makosa hayo ni; la kwanza ni ufujaji na ubadhirifu wa fedha za chama zaidi ya Sh. milioni 1.2 kinyume na kifungu cha 28(2) cha sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa sura 329 marejeo ya mwaka 2019 kikisomwa pamoja na aya 21 jedwali la kwanza pamoja na vifungu vya 57(1)na 60(2) vya sheria ya uhujumu uchumi ya sura ya 200 marejeo ya mwaka 2019.

Kosa la pili alidai kuwa ni la wizi wa wakala kinyume cha vifungu namba 265 na 273(b) vya sheria ya kanuni za adhabu sura namba 16 marejeo ya mwaka 2019.

Alidai mshtakiwa huyo alifikishwa mahakamani hapo kwa mara ya kwanza Januari 5, mwaka jana, akikabiliwa na mashtaka hayo kwa kutoa Sh. milioni 1.2 kwenye akaunti ya Kidema (AMCOS) na kuzitumia kwa matumizi yake binafsi badala ya kulipa ushuru kwenye akaunti ya Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Simiyu (SIMCU 2018 LTD).

Mshtakiwa huyo alipopewa fursa ya kujitetea ili mahakama isipewe adhabu, alidai kuwa wakati ametoa fedha hizo benki kwenye akaunti ya Kidema AMCOS, ghafla alivamiwa na operesheni iliyokuwa ikiendeshwa na Meneja wa Kampuni ya Bilchad, kuporwa na kutoroka nazo.

Alipotakiwa kuthibitisha madai yake hayo mbele ya mahakama hiyo kwa kutoa ushahidi alishindwa hivyo na kutiwa hatiani na kuhukumiwa kifungo hicho jela.



Mkazi wa Kata ya Bukooba Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Salome Michael, akielezea alivyotolewa katika mpango wa kunusuru kaya maskini wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwa kuanzisha shughuli za kumwingizia kipato katika miradi inayoendelea kwa kigezo cha umri, wakati wa mkutano wa hadhara ulioitishwa na Mbunge wa Kahama, Jumanne Kishimba (hayupo pichani), jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

## CHADEMA yatamba kushinda mitaa 81 Tarime Mjini

**Na Timothy Itembe,** TARIME

CHAMA cha Demokokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimetamba kuwa kitatwaa mitaa yote 81 ya Jimbo la Tarime Mjini mkoani Mara katika uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika nchini baadaye mwaka huu nchini.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa CHADEMA Tarime Mjini, Selemani Abdalah baada ya chama hicho kutangaza kuwa kimeanza kufanya maandalizi kwa ajili ya uchaguzi huo ili kuhakikisha kinafikia malengo waliyojiwekea, ikiwamo kutwaa mitaa hiyo jimboni humo.

Abdalah, alisema chama hicho kinawakaribisha wanachama wake kujitokeza kwa wingi kuchukua fomu kwa kuwa ni haki yao kidemokrasia na si kukumbatia mgombea mmoja.

Kuhusu nafasi ya ubunge jimboni humo, Abdalah alisema inawaniwa na wanachama mbalimbali akiwamo yeye na Bobu Wangwe ambaye tayari ametia nia.

Aliwataka watia nia wengine kuchangamkia nafasi hiyo kwani milango bado iko wazi.

Mwenezi wa CHADEMA Tawi la Makire, Butiku Masaku, alisema chama hicho kimetoa nafasi kwa wanachama wote wenye nia ya kugombea nafasi katika uchaguzi huo wa serikali za mitaa na mkuu mwakani kujitokeza mapema iwezekanavyo.

Mwanachama wa chama hicho, Rukia Msugiri aliwaomba wanawake kujitokeza kugombea nyadhifa mbalimbali katika chaguzi hizo ili kuwa na usawa wa kijinsia.

Aidha, hadi sasa wanawake 162 wamejitokeza kugombea nafasi mbalimbali katika uchaguzi wa serikali za mitaa, 48 udiwani na wengine wawili ubunge.

# Adaiwa kutoa mimba, kutupa kichanga chooni

**Na Ambrose Wantaigwa,** BUNDA

MWANAMKE ambaye jina lake halijafahamika anadaiwa kutoa ujauzito na kutupa kichanga kwenye choo kilichoko Mtaa wa Makumbusho Kata ya Nyasura Halmashauri ya Mji wa Bunda mkoani Mara.

Mashuhuda wa tukio hilo, wakizungumza na NIPASHE, walidai kuwa mwanamke huyo alitekeleza ukatili huo juzi majira ya asubuhi.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo juzi, Mwenyekiti wa Mtaa huo, Boniphase Musiba, alisema mwanamke huyo, amekamatwa kwa kushirikiana na wananchi na kukabidhiwa Jeshi la Polisi kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

Musiba, alisema serikali ya mtaa huo inakemea tukio hilo kwa kuwa linaharibu taswira yake na ni kinyume na taratibu za wananchi wanaokuwa katika mahusiano.

"Kama mzazi mmojawapo akiona hana utayari wa kujifungua ni afadhali atumie njia mbadala ikiwamo usuluhishi na uzazi wa mpango ili kuepuka madhara kwa watoto wanaotarajiwa, " alisema.

Diwani wa Nyasura, Magigi Samwel, alisema matukio ya utupaji wa watoto na utoaji mimba yameanza kukithiri siku za hivi karibuni katika maeneo yao na kuitaka jamii kuacha vitendo hivyo.

Aliwataka wanandoa wanaokabiliwa na migogoro kutoa taarifa ofisi ya ustawi wa jamii au ofisi za serikali za mitaa badala ya kujichukulia hatua za kutupa vichanga kwa kuwa ni kosa kisheria.



Ukurasa 12

**Kufeli darasani si kushindwa maisha, ukikwama umekosa nia kusonga mbele**



Ukurasa 13

Yatinga kanisani na msikitini, shule sekondari, msingi zaguswa



Ukurasa 14

**Wanufaika wa TASAF na simulizi kuuaga ufukara**


Nipashe TESA

Jumanne Agosti 6, 2024

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI


ELIMU

NA BEATRICE PHILEMON

# Fahamu ujasiriamali ni zaidi, si fedha pekee unazotamani kwa wateja

ANAYETAKA kufanya biashara au kuwa mjasiriamali, akumbuke kuwa ujasiriamali ni zaidi ya kupata pesa, mfanyabiashara lazima ajitahidi kutatua changamoto za watu katika eneo analoishi ndipo atapata fedha anazotamani kutoka kwa wateja wanunuzi wa bidhaa na huduma zake.

Anasema Janeth Makwenjula, Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa CCM, Wilaya ya Ulanga, anayeanzisha kampeni ya mafunzo kwa wananchi kuanzia kinamama, wanaume na vijana, kujenga jamii ya wajasiriamali na watu wanaotamani mabadiliko.

Anasema anachukua hatua hiyo, baada ya kugundua kuwa idadi kubwa ya wanakijiji cha Milola wanaishi kwenye hali ya umaskini, wapo nyuma kimaendeleo, hawajui kuanzisha wala kuendesha hata biashara ndogo.

"Niliamua kuwafundisha elimu ya biashara, ujasiriamali, ukatili kijinsia, haki za wanawake na wapi pa kuzipata, mikopo kutoka taasisi mbalimbali za kifedha pamoja na ya halmashauri," anasema Janeth.

Anaeleza kuwa baada ya kupata mafunzo kutoka shirika la kiraia la 'Women Action towards Entrepreneurship Development (WATED), anaamua kuendeleza kile alichopata kwa kuwapa wengine.

Anasema wakati wa kutoa mafunzo, anawazungukia watu vijijini na kutoa elimu kwa wanawake, vijana na wanaume kuhusu ujasiriamali, elimu ya biashara, haki za wanawake, unyanyasaji wa watoto, ukatili wa kijinsia kwa watoto, wanawake na pia kuwaunganisha na taasisi zinazotoa mikopo.



Biashara na ujasiriamali vijijini. **PICHA MTANDAO**

### MAFANIKIO

Kutokana na elimu waliyopata, hali ya maisha ya wananchi Milola imebadilika tofauti na miaka ya nyuma ambapo wanawake wengi walikuwa wakifanya vibarua hasa kupalilia mashamba ambako walipata hela kidogo.

Wanawake wengi hivi sasa katika Kata ya Igumbilo, Milola, Lupilo na vijiji kama Mavimba wameanzisha biashara ndogo za mamalishe, kuuza mkaa, migahawa, kilimo cha mboga na wanaume wameanzisha maduka na wengine wanauza samaki mitaani.

Lakini pia wanawake wamechukua mikopo, kuanzisha biashara ya mgahawa ili kujiongezea kipato, kusaidiana na waume zao katika majukumu mbalimbali ya kifamilia na kupunguza kutegemea wanaume zao kwa kila kitu.

"Hadi sasa nimetoa mafunzo katika kata 21 za Wilaya ya Ulanga, na kwa upande wa haki za wanawake, 14 kati ya 16 waliokuwa wamepigwa na kutelekezwa na waume zao wamepata haki zao na asilimia kubwa ni jamii ya wafugaji." Anasema Janeth.

Lakini, pia hivi sasa wanawake wengi wana mali zao, wamejenga nyumba zao, watoto wao wanapata matunzo kutoka kwa baba zao tofauti na miaka ya nyuma.

Kilasi Michael ni mmoja wa walionufaika na mafunzo ya Janeth ni mkufunzi kutoka kampuni ya Madeo Finance, anawashauri watu kuwa wakitaka kuwa wajasiriamali au wafanyabiashara, ni lazima kuangalia eneo wanaloishi kuna changamoto gani inayowakabili wananchi.

Anasema wakishaitambua wanaweza kuanzisha mradi au biashara ambayo itaweza kutatua changamoto zilizopo na hatimaye waweze kufanikiwa au kujiongezea kipato. Pia, wanapaswa kuwa na maono ya biashara kwa sababu yatawezesha kumwongoza afanye nini na kwa muda gani, anasema na kuongeza.

Mbali na hilo, wakati wa kuanzisha biashara yake au mradi, lazima ajiulize kuwa anataka kuwa nani, lini na tena kufanya nini baadaye, lakini pia afanye bidii kufikia maono ya biashara yake kwa sababu wajasiriamali waliofanikiwa ni wale walioweza kubadili maono yao kuwa uhalisia.

"Pia afanye biashara yake tofauti, aiboreshe kila siku, afanye bidhaa zake vizuri na kila mara akumbuke kuwa ushindani ni mkubwa sokoni katika hivyo ajitahidi kuongezea tija, ubora wa huduma kwenye bidhaa anazouza.

Vile vile, atumie pesa vyema, "Tumia pesa kwa mpangilio na lazima uchuje vitu vya kutumia ili mtaji wako ukue," anasema Michael.

Anakumbusha kujitahidi pia kufahamu wateja wake na kuwajali ajue wanataka nini, kusikiliza maoni na ushauri wao, kuhakikisha anakamilisha mahitaji yao, kutumia lugha nzuri na rafiki kwa wateja tena amfanye mteja aone anamthamini na anatanguliza huduma kabla ya pesa, anashauri.

### KUTUMIA TEKNOLOJIA

Michael anawashauri wajasiriamali wajifunze kutumia teknolojia, mitandao ya biashara na kusoma magazeti, majarida na vipeperushi ili kupata taarifa, ujuzi, maarifa na wateja, kadri tekinolojia inavyokuwa.

"Ndivyo unavyoweza kutangaza bidhaa zako, kupata wateja wapya na biashara kupanuka zaidi," anasema.

Anasema zama hizi ujasiriamali usipuuze nafasi ya teknolojia kwa sababu ndicho kinachosukuma maendeleo mbele na watu wanaishi kwenye dunia ya sayansi na teknolojia.

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA HALFANI CHUSI

# Kufeli darasani si kushindwa maisha, ukikwama umekosa nia kusonga mbele

IKO misemo kadhaa inayozungumzia elimu mathalani, kufeli shule si kushindwa maisha, ujumbe unaolengwa kukumbusha kuwa ikiwa umefanya vibaya darasani usisononeke.

Aidha, msemo unakutia moyo kuwa mtu ana nafasi ya kufanikiwa kimaisha hata nje ya darasa na hicho ndicho kinachothibitishwa na mabinti kadhaa jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

Waliofeli shule wana nafasi bado anasema Mkurugenzi wa Taasisi ya Panda Initiative Rehema Sanga, anapozungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam.

Anakumbusha kuwa ukifeli kwenye elimu jumuishi darasani unaweza kuingia katika mafunzo ya ufundi, kupata fani mbalimbali na hatimaye ukazitumia kuendesha maisha yako.

Kwa kutumia jicho hilo, unaweza kusema ndiyo maana leo wapo wataalamu wengi wenye ujuzi kuanzia mafundi pikipiki, magari, umeme, mitindo ya mavazi, urembo na upishi wanaoendesha maisha yao kupitia taaluma za mafunzo ambazo wakati mwingine hazitokani na kufaulu mtihani shuleni.

Anaongeza taasisi yake inawawezesha na kuwainua wasichana na makundi maalumu kupitia mradi wa Wezesha Binti, kuwaunga mkono waliofeli shule ama kushindwa kusoma kwa sababu mbalimbali.

Anasema imewapatia mafunzo ya cherehani mabinti 23 ambao karibuni wamehitimu na kupewa vyeti na Mkuu wa Wilaya ya Ilala Edward Mpogolo.

Mabinti na jamaa zao wanalitafsiri jambo hilo kuwa ni sawa na kuvushwa katika giza na kuingia kwenye mwanga.

Siku hiyo nyuso za mabinti hao zilitawaliwa na tabasamu kuonyesha kuwa walioko mtaani wanaweza kubadili upya ndoto zao na kuwa walezi bora wa familia na hata kuondokana na utegemezi kwa kupatiwa mafunzo katika fani mbalimbali.

Mkurugenzi wa Panda Initiative Rehema, anaitaka jamii na wadau kununua bidhaa zinazozalishwa na mabinti 23 waliohitimu mafunzo ya ufundi cherehani popote walipo.




Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo , akimkabidhi cheti mmoja wa wahitimu waliofadhiliwa na Panda Initiatives. Kushoto ni Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Rehema Sanga. **PICHA: HALFANI CHUSI**

> Binti akipata shida mtoto wake ataishi maisha bora kupitia mfumo huo, ambao taasisi ya Panda imeufanya.

Anatoa ujumbe kwenye mahafali ya mabinti hao yanayofanyika Kivule yaliko makao makuu ya Panda Initiative.

Rehema anasema mradi huo wa Wezesha Binti lengo lake ni kuboresha hali ya uchumi ya wasichana na wanawake vijana katika kata ya Kivule kwa kuwapatia elimu hasa ujasiriamali na ufundi.

Anaongeza kuwa mabinti hao watasaidia kukuza uchumi wao na taifa na kwamba bidhaa watakazo zalisha zitauzwa nje na ndani ya nchi hata kufikia soko la kimataifa sambamba na kuongeza ajira.

"Tunaomba wafadhili wengine wajitokeze kuendelea kufadhili mradi huo, hatupokei ruzuku, hatuna vyanzo vingine vya fedha tunaomba misaada ili tuwakomboe vijana.

"Serikali iwaunge mkono kwa kununua bidhaa walizotengeneza wachangiwe katika kuanzisha kiwanda chao kidogo na kikundi chao cha Komboa Women Group," anasema.

Rehema, anaungwa mkono na Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, anayezitaka taasisi mbalimbali kuwashika mkono mabinti wengine kwa kuwapa mafunzo katika fani nyingine zaidi ili wajiepushe na mambo yasiyofaa.

Mpogolo aliyekuwa mgeni rasmi katika mahafali hayo, baada ya kuwakabidhi vyeti, anawataka wahitimu hao kwenda kuendeleza mema na kuchangamkia fursa ili waweze kupata matunda ya walichokisomea.

Aidha, anaahidi kuwasaidia kupata mkopo wa asilimia 10 unaotolewa na halmashauri kwa ajili ya wanawake, wenye ulemavu na vijana, mabinti hao 23 waliohitimu mafunzo hayo.

Anasema watapata kipaumbele kwa ajili ya kuwainua vijana kwa vile tayari wana kikundi ambacho ni moja ya kigezo cha kupata mkopo huo kiurahisi.

Binti akipata shida mtoto wake ataishi maisha bora kupitia mfumo huo, ambao taasisi ya Panda imeufanya.

Anaongeza kuwa inawezekana kuwakwamua kiuchumi, akawahakikishia kuwa atashirikiana ili wapate msaaada lakini pia kutafuta wahisani wengine.

Anaahidi kuangalia namna ya kuchangia cherehani mbili za umeme akisema mabinti 23 ni familia kubwa huwezi kuzikuta kwenye madanguro.

Anazungumzia kupambana na madanguro akisema lazima kuanze na kumkomboa mwanamke kwa kumwezesha kiuchumi kama ilivyofanyika kwa mabinti hao.

**WAHITIMU**

Wahitimu walipopokea vyeti walionyesha taswira kuwa huko mtaani wapo mabinti wengine ambao wangetamani kutabasamu kama ilivyo kwa hao wengine, lakini hawajapata nafasi.

Mhitimu wa mafunzo hayo, Josephine Michael, anaishukuru Taasisi ya Panda Initiatives kwa kuwawezesha kupata mafunzo akibainisha kwamba yatawawezesha kupambana na umaskini.

"Nilichaguliwa katika mafunzo ya ushonaji baada ya kushindwa kumaliza kidato cha nne, nilifanya majaribio nikafaulu nikapata nafasi ya kufadhiliwa ninashukuru sana.

"Nimejifunza kushona nguo za aina zote, nisingekuja kusoma nisingejua kitu chochote kwa sasa hata kushona suti ninajua ninatoa wito kwa mabinti wengine walioko mtaani wachangamkie fursa kama hizi zinapotokea.

Mhitimu mwingine, Masaa Warioba, anasema baada ya kumaliza kidato cha nne alipata taarifa kwa mjumbe wa serikali ya mtaa wake kuhusu taasisi hiyo kusaidia mabinti kupata mafunzo akachangamkia fursa.

"Tupo tayari kufanya kazi kwa kujiriwa au kujiajiri pia. Kama kuna mtu anahitaji mtu wa kushona tupo tayari tuna mafunzo tuliyoyapata kutoka kwa wataalamu, kwa hiyo tunaomba wadau mbalimbali na serikali watukumbuke zinapotokea fursa za ushonaji," anasema Masaa.

## Fahamu ujasiriamali ni zaidi, si fedha pekee unazotamani kwa wateja

**INATOKA UK.11**

Anasema zama hizi ujasiriamali usipuuze nafasi ya teknolojia kwa sababu ndicho kinachosukuma maendeleo mbele na watu wanaishi kwenye dunia ya sayansi na teknolojia.

Anataja simu, kompyuta, mtandao wa internet, ya biashara na tovuti na kwamba vyote vikitumika vinaweza kuwafikia watu wengi zaidi na kuongeza mauzo ya huduma au bidhaa unazozalisha.

Pia wajasiriamali wawe karibu na wateja wao ili kutatua shida na mahitaji yao na pia watie bidii kujifunza mbinu bora za kufanya biashara kupitia mitandao na majukwaa mbalimbali.

"Vile vile, lazima wawe na biashara moja ambayo wana maono nayo. Chagua watu wa kushirikiana nao, kwa mfano mfanyakazi lakini awe na uwezo wa kazi, usichukue yeyote eti ni rafiki au mtoto wa dada, au wa rafiki hapana angalia ambaye yuko tayari kufanya kazi na wewe kwa moyo na kufikia mafanikio," anasema.

ELIMU
NA SABATO KASIKA, BAGAMOYO

KAMPENI DAWA ZA KULEVYA

# Yatinga kanisani na msikitini, shule sekondari, msingi zaguswa



Elimu ikitolewa kwa wanafunzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

RIPOTI ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kukabili Dawa za Kulevya na Uhalifu, (UNODC), inataja idadi ya waraibu wa dawa za kulevya duniani kuwa ni milioni 292.

Kiwango kikiongezeka zaidi ya idadi ya mwaka 2022 ikiwa ni ongezeko la asilimia ishirini katika kipindi cha miaka 10 iliyopita.

Akizindua ripoti ya mwaka huu, mwezi uliopita huko Vienna Austria, Mkurugenzi Mkuu wa UNODC, Ghada Waly anaeleza kuwa, kuzalisha dawa za kulevya na kuzitumia kunazidisha hali ya kukosa utulivu, usawa, amani na madhara makubwa ya kiafya, usalama pamoja na ustawi duniani.

"Tunahitaji kutoa matibabu yaliyofanyiwa uchunguzi na kuwa na ushahidi wa kusaidia waathirika huku tukilenga kuondoa soko haramu la dawa hizo na kuwekeza zaidi kuzuia matumizi yake." Anasema Ghada.

UNODC inasema, bangi inatumika zaidi duniani kote ambako kuna watumiaji milioni 228, lakini uzalishaji wa cocaine umeweka rekodi mpya ya juu ukifikia tani 2,757 mwaka 2022, ikiwa ni ongezeko la asilimia 20 zaidi tangu mwaka 2021.

Ingawa wastani wa watu milioni 64 duniani kote wanakabiliwa na matatizo yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya, ni mtu mmoja kati ya 11 anayetibiwa. Anasema, Mkurugenzi Mkuu wa UNODC.

Ripoti ya UNODC inaigusa Tanzania na dunia nzima kwa ujumla, ndiyo maana inaanza kufanyiwa kazi Bagamoyo mkoani Pwani, wadau wakitoa elimu kwa waraibu kujua haki zao, kujua madhara ya dawa hizo, pia kuelimisha jamii kuacha unyanyapaa kwa waraibu ili wapewe huduma zote za msingi zinazotakiwa.

Aidha, waraibu, wanafunzi, walimu, wazazi, viongozi wa dini, serikali, polisi, madaktari, wanasheria na maofisa wa ustawi wa jamii wilayani humo wanahusishwa.

Shirika la kiraia linalohudumia waraibu wa dawa hizo la Life and Hope Rehabilitation Organisation (LHRO), linalofanya mradi huo, kwa kuwezeshwa na mfuko wa kimataifa uitwao U.S. Ambassador Fund for HIV/AIDS Relief (AFHR Grant) and Pepfar.

Mwalimu mlezi wa Shule ya Msingi Kizuiani Bagamoyo, Raphia Azza, ambaye mradi huo upo shuleni kwake, anasema wana vipindi maalumu vya kuelimisha wanafunzi kuhusiana na madhara ya dawa za kulevya, na ujio wa LHRO umewaongezea ujuzi na nguvu zaidi.

"Tunatenga muda kuwafundisha kujiepusha na dawa hizo, shirika la LHRO limetuongezea elimu hii, kwani ni wabobezi kwa mbinu mbalimbali za kutambua vyanzo vya vijana kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya," anasema Raphia.

LHRO wamewafundisha umuhimu wa kuzingatia malezi, kujua tabia za wanafunzi na kufuatilia mienendo yao na kuwaepusha na makundi hatarishi na ya kihalifu. Aliyekuwa mraibu Zaka Nchimbi, anayeishi Kata ya Kisutu wilayani Bagamoyo, ambaye ni dereva wa bodaboda, anasema elimu hiyo imemtoa kwenye dawa hizo.

"Nilishtuka mapema baada ya kuelimishwa kujua haki zangu na madhara ya dawa hizo, sasa ninatumia dawa ya methadone huku nikiendelea kufanya kazi yangu," anasema Nchimbi.

Kiongozi wa Msikiti wa Wazee Magomeni, Ustadhi Haji Mwinyi, amefikiwa na LHRO anasema, elimu hiyo imekuja wakati sahihi na kwamba wamekuwa wakitoa nafasi kwa waelimishaji wa shirika hilo wakati wa mawaidha kuzungumza na waumini.

"Dawa hizi zimeharibu vijana wengi. Baada ya kupata elimu hii, tumekuwa tukitumia kipindi cha mawaidha, kukumbusha waumini kuzingatia malezi mema ya watoto wao," anasema Ustadhi Mwinyi.

Mchungaji wa Kanisa la Mlima wa Sayuni Mathayo Mwanjisi, anasema, elimu hiyo inatolewa kanisani kwake, na kwamba kilichobaki ni kuendelea kuliombea taifa ili vijana waache dawa hizo na umma ubadilike.

Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Bagamoyo, Mushana Mujema anasema, hatua ya shirika hilo kuihusisha polisi katika mradi huo ni nia halisi ya kutaka kusaidia vijana kuacha dawa hizo.

Anasema, wanazuia vitendo vyote vya uhalifu, kwa kuwa baadhi ya vijana wanaotumia dawa hizo ni wahalifu na kwamba wataendelea kushiriki katika kutoa elimu ili kusaidia vijana kuacha maisha ya uraibu wawe msaada kwa familia, jamii na taifa kwa ujumla. Mganga Mkuu wa hospitali ya wilaya hiyo, Dk. Kandi Lussingu, anapongeza viongozi wa LHRO kwa kuanzisha mradi huo na kufafanua kuwa umeibua waraibu wengi zaidi wanaofika hospitalini hapo kwa ajili ya kutibiwa na methadone.

Anaongeza kuwa, miaka ya nyuma kulikuwa na idadi ndogo ya waraibu wanaofika kunywa dawa, na kuongeza kuwa sasa wamefikia zaidi ya 700, na kwamba hatua hiyo inaonyesha ni jinsi gani elimu imewasaidia.

> Dawa hizi zimeharibu vijana wengi. Baada ya kupata elimu hii, tumekuwa tukitumia kipindi cha mawaidha, kukumbusha waumini kuzingatia malezi mema ya watoto wao.

"Niwashukuru viongozi wa idara ya maendeleo ya jamii, polisi kata, dawati la jinsia na wadau wengine kwa kushirikiana na LHRO kuwatoa vijana katika uraibu wa dawa za kulevya," anasema Dk. Kandi.

Anaeleza kuwa, ni muhimu vijana waelimishwe, watambue madhara ya dawa za kulevya ili waachane nazo, pia wapewe elimu ya ujasiriamali pamoja na mtaji ili waweze kujishughulisha na shughuli za kuwaingizia kipato.

**LHRO KAZINI**

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRO, Al-Karim Bhanji, anasema, mradi wa kutoa elimu hiyo, ulianza Desemba mwaka jana na kwamba awamu ya pili ya mradi huo imeishia Julai na sasa wanaingia awamu ya tatu ambayo itaishia Desemba mwaka huu.

Bhanji anaongeza kuwa tangu waanze kutoa elimu, wamefika katika Shule za Msingi Kiromo na Jitegemee, Kizuiani na Nianjema na sekondari za Mwambao na Asanary. Aidha, wamekifikia kituo kidogo cha polisi Magomeni, hospitali ya wilaya, zahanati za Kiromo, Buma na maskani ya Buma na vijiwe vya bodaboda.

Mbali na hapo anasema, wameyafikia Makanisa ya Katoliki Parokia ya Mtakatifu Elizabeth, Kanisa la Mlima wa Sayuni lililoko Dunda, Kanisa la Mungu Baba lililoko Nianjema na la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na vijiwe mbalimbali vya waraibu wa dawa hizo.

Bhanji anasema, wametinga misikiti ya Masjid Rahman, Msikiti wa Wazee Kata ya Magomeni, Masjid Noor na Masjid Rahman ulioko Kata ya Dunda.

Anafafanua kuwa, njia wanayotumia kutoa elimu ni mikutano ya hadhara vijijini, kwenda shuleni kuzungumza na walimu na wanafunzi na kwenye nyumba za ibada.

Anasema wanatamani kuona jamii ikibadilika, waraibu wakitambua athari na kuacha dawa hizo, pia wakifahamu haki zao akisema kumekuwa na unyanyapaa, unaofanywa na wanafamilia na jamii wakiwachukulia kama wasiofaa.

Kundi hilo anasema linatakiwa kusaidiwa, ndio maana wanatoa elimu, wasinyanyapaliwe, watambue haki za kupata tiba na kuachana na dawa hizo tena wanufaike na huduma nyingine za kijamii kama fursa za kiuchumi, miradi ya maendeleo na ujasiriamali.

ELIMU

NA RESTUTA JAMES




Mnufaika wa TASAF Shufaa Mfinanga, mkazi wa Kilimani Manispaa ya Moshi akiwa gengeni kwake. **PICHA: RESTUTA JAMES**

# Wanufaika wa TASAF na simulizi kuuaga ufukara

TAKWIMU za sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, zinaonesha kwamba idadi ya Watanzania ni milioni 61. Kati yao, asilimia nane wanaishi katika wimbi la umaskini, wakishindwa kumudu milo mitatu kwa siku, makazi na mavazi.

Asilimia hiyo ni sawa na Watanzania 5,195,605 wanaoishi katika umaskini uliokithiri au mafukara ambao kwa uwiano asilimia 55.7 ni wanawake na 44.3 wanaume.

Ili kuliondoa kundi hilo kwenye lindi la umaskini, serikali ilianza kutekeleza mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), kuanzia mwaka 2000, ikiwa ni moja ya mbinu ya kuzinusuru kaya zinazoishi katika mstari wa umaskini.

Katika jitihada za kuzikwamua, serikali imekuwa na mipango kadhaa ukiwamo ule wa utoaji wa ruzuku ya fedha taslimu kwa kaya hizo kila mwezi na utekelezaji wa miradi muhimu ya huduma za kijamii kama afya na elimu.

Mipango hiyo imeonesha mafanikio katika sekta za afya, elimu na kuongezeka kwa rasilimali katika kaya. Matokeo hayo chanya yamepanua afua za TASAF, kiasi cha kuwa ni mfumo wa kinga ya jamii tangu mwaka 2012, yakilenga kuziwezesha kaya maskini kuongeza vipato na fursa za kujikimu.

Ni afua hizo ambazo zinahitimisha kipindi cha pili cha TASAF awamu ya tatu kinachofikia tamati mwakani. Aidha, mpaka sasa ni takribani kaya 400,000 zilizonusuriwa kutoka kwenye ufukara hadi kumudu mahitaji yote ya msingi pamoja na kuweka akiba. Kaya hizo ni zile zinazohudumiwa na TASAF kutoka Halmashauri 187, Tanzania Bara na Visiwani.

Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Shedrack Mziray, anaanza kwa kueleza kuwa, madhumuni ya kipindi cha pili katika awamu hii ni kuongeza fursa za kujiongezea kipato na kuboresha huduma za kiuchumi na kijamii kwa kaya za walengwa na kulinda masilahi ya watoto wao.

Anasema mfuko huo umejikita katika kuzikwamua kaya za walengwa kupitia maeneo matatu ambayo ni ruzuku ya fedha kwa wanufaika ili kujiongezea kipato na kuwekeza katika afya na elimu ya watoto.

Mziray anasema ili kuinua uchumi wa kaya, mfuko huo unazijengea uwezo katika utunzaji wa rasilimali, kutengeneza njia mbadala na endelevu za kipato na ajira za muda mfupi mathalani kwa kushiriki katika kazi za jamii.

"Kwenye ile miradi ambayo inaibuliwa na jamii katika ngazi ya kijiji au mtaa, kaya zenye watu wenye uwezo wa kufanyakazi tunawawezesha kuitekeleza ili kupata ujuzi na stadi za maisha," anasema Mziray.

Mziray anasema mikakati hiyo imefanikisha kaya 400,000 kuondoka kwenye ufukara (umaskini uliokithiri), baada ya kufanikiwa kumudu huduma za msingi za chakula, makazi na mavazi. Zikifanikiwa kujenga nyumba na kuziwekea umeme na kuanzisha miradi ambayo inawahakikishia kipato cha muda mrefu.

Anasema, kaya hizo zinaondolewa kwenye mpango baada ya kufanyiwa tathmini na kujiridhisha kwamba zinaweza kujitegemea.

"Kaya hazitakiwi zikae kwenye mpango milele. Utaratibu unataka kwamba, tukishawatambua tuwaondoe kwenye umaskini uliokithiri. Tunawawezesha kiuchumi, kukuza kipato cha kaya na kutengeneza rasilimali watu kupitia utekelezaji wa miradi ya ujenzi inayowapa stadi za maisha," anasema Mziray.

Kwa mujibu wa Mziray, kipindi cha pili cha TASAF awamu ya tatu kilichoanza mwaka 2020 hadi 2025, kinagharimu Sh. trilioni mbili, ambazo ni mkopo wa Dola za Marekani 650 kutoka Benki ya Dunia (WB) na michango ya wadau wa maendeleo kutoka Jumuiya ya Ulaya (EU), Mashirika ya Umoja wa Mataifa (UN), Sweden, Ireland, Norway na Dola milioni 50 kutoka Umoja wa Nchi zinazouza zaidi mafuta duniani (OPEC).

Mkurugenzi wa Mradi wa TASAF, John Stephen, anasema kaya zinazoondolewa zinapatiwa ruzuku ya Sh. 350,000 kwa ajili ya kuanzisha mradi utakaoziingizia kipato cha uhakika kwa muda mrefu.

Anasema kaya 83,666 zimepewa Sh. bilioni 17.1 kama ruzuku ya tija ya kujikimu, mafunzo na ushauri wa biashara ambazo zimefanikiwa kuanzisha miradi midogo ya kuwaingizia kipato.

Anataja baadhi ya miradi hiyo kuwa ni ufugaji wa nguruwe, kuku wa nyama, njiwa wa mapambo, mbuzi, uanzishaji wa biashara ndogo kama za genge, uuzaji wa gesi ya kupikia na kilimo cha bustani.

"TASAF inasaidia uwekezaji huu kwa ujuzi wa kukuza biashara na mafunzo ya kiufundi. Jumla ya vikundi vya akiba vya wanufaika 60,327 vyenye wanachama 838,241 vimeundwa. Kiasi cha akiba katika vikundi ni Sh. 7.9 bilioni. Kati ya akiba hizo, Sh. bilioni 3.2 zimetolewa kama mikopo kwa wanachama kwa ajili ya kuwekeza katika shughuli zao za kuwaingizia kipato," anasema.

### KAULI YA WANUFAIKA

Baadhi ya wanufaika wa ruzuku ya uzalishaji, katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, wameonyesha ubunifu kwa kuanzisha miradi ya ufugaji, ushonaji na biashara ndogo.

Mkazi wa Mtaa wa Kariwa Chini, Kata ya Rau, Caroline Minja, anasema, alijiunga na TASAF mwaka 2015 akiwa anaishi kwenye chumba kimoja cha udongo na watoto wake watatu na kwamba ruzuku ya kila mwezi imemwezesha kununua mahitaji ya watoto na kujenga nyumba ya kuishi.

Anasema TASAF imempa mafunzo ya namna ya kutunza fedha, kuendesha biashara na kuikuza jambo lililomwezesha kufuga nguruwe, kuanzisha kilimo cha bustani na genge linalomwingizia kipato kila siku.

"Kama mnavyoona nimejenga nyumba ya vyumba viwili kwa matofali ya kuchoma, ina umeme na nimefanikiwa kuanzisha genge kwa ajili ya kipato cha kila siku. Nimejiunga pia na kikundi cha kuweka na kukopa ili niendelee na nidhamu ya kutunza fedha," anasema.

Anasema mtoto wake mmoja, amefanikiwa kusoma hadi chuo kikuu na amepata mkopo kwa asilimia 100 baada ya TASAF kumtambulisha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Mkazi wa Mtaa wa Sabasaba katika Kata ya Rau, Lucy Tenga, anasema ruzuku ya uzalishaji imemwezesha kuanzisha mradi wa kufuga kuku wa nyama ambao unamwingizia kipato cha uhakika kila baada ya wiki nne.

"Watoto nao wamesoma na nimejifunza kuweka akiba. Ninachoweza kusema ni kwamba fedha kidogo inaweza kutupeleka mahali pazuri, kwa sababu ruzuku tuliyokuwa tunapewa haikuwa kubwa lakini baada ya mafunzo kutoka kwa wataalamu tumejua kutumia na kuweka akiba," anasema.

Selina Msofe, anasema amefanikiwa kujenga nyumba na kuweka maji na umeme, pia anafuga nguruwe na kuku ambao wanamwingizia kipato cha uhakika.

"Umaskini sasa kwa heri. Kwa sasa nafuga kuku na nguruwe. Nilianza na nguruwe mmoja, akazaa nikauza nikajenga banda la pili kisha nikaongeza zaidi. Baadaye nikajenga banda la kuku ambapo nao wananiingizia kipato," anasema.

Kama walivyo wanufaika wengine, Anna Raphael, mkazi wa Sabasaba katika Kata ya Kiborloni, anasema ruzuku ya TASAF imemwezesha kufuga njiwa wa mapambo ambao wanamwingizia kipato kikubwa.

"Njiwa hawa, jozi inauzwa kati ya 250,000 hadi 300,000. Nimejenga nyumba kama mnavyoona na nafuga kuku na njiwa. Nimeondoka kwenye aibu ya kukosa mlo na sasa naweza kusimama mbele za watu. Tumefundishwa utaratibu mzuri wa kuhakikisha tunaweka akiba kila wiki kupitia vikundi tulivyounda," anasema.



## Polisi yawekwa sawa uchaguzi wa mitaa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

ASKARI wa Jeshi la Polisi wametakiwa kutambua wajibu wao tangu kuanza kwa uchaguzi wa serikali za mitaa hadi kuapishwa kwa viongozi watakaochaguliwa na wananchi ili usikumbwe na changamoto.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Mjumbe wa Dawati la Uchaguzi Taifa Kamishna Msaidizi wa Polisi, Lupisio Mwakyusa kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai nchini, wakati akitoa elimu ya uchaguzi kwa maofisa, wakaguzi na askari wa jeshi hilo wilayani Manyoni Mkoa wa Singida.

Mwakyusa, alisema wajibu wa polisi katika uchaguzi huo ni pamoja na kulinda mikutano ya kampeni, wagombea, viongozi wa serikali kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), vifaa vya kupigia kura, wapigakura na miundombinu mingine ya uchaguzi.

Alisema askari wanatakiwa kuzisoma na kuzielewa vizuri sheria, kanuni na miongozo ya uchaguzi huo ili iwe rahisi kwao kuzitekeleza, hivyo uchaguzi kufanyika kwa amani na utulivu.

Kwa upande mwingine, Mwakyusa, aliwataka wananchi wenye sifa za kupigiwa au kupiga kura kujiandaa kuchagua viongozi au kugombea kwenye uchaguzi huo utakaofanyika nchini baadaye mwaka huu.

"Kila mwananchi mwenye sifa ya kupiga au kupigiwa kura anao wajibu wa kuzifahamu na kuzifuata sheria, taratibu na miiko ya uchaguzi tangu kuanza kwa mchakato hadi kuapishwa kwa washindi," alisema.

Kamishna Msaidizi wa Polisi, Elisante Olomy kutoka Makao Makuu ya Polisi Kitengo cha Polisi Jamii, aliwataka wananchi wanaotarajia kugombea nyadhifa mbalimbali za uongozi kutojiingiza katika imani za kishirikina kwa kuamini watashinda uchaguzi.

# Bomoabomoa yanukia Dodoma

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imetoa siku 14 kwa wakazi wa Mtaa wa Chikowa uliopo Kata ya Mbabala waliovamia eneo lililotengwa kuotesha miti kuvunja nyumba zao, kusitisha shughuli za kilimo na kuondoka mara moja.

Amri hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi wa Jiji hilo, John Kayombo, wakati wa kikao baina yao na wakazi hao ambacho kilikuwa mahususi ili waondoke kwenye eneo hilo lenye ukubwa ekari zaidi ya 896 ambalo lililotengwa kwa uoteshaji wa miti tangu 1972.

Kayombo, alisema amri hiyo imetolewa kwa wakazi hao kwa kuwa serikali ina hati miliki ya eneo hilo kwa ajili ya kuotesha miti kutoka mwaka 1972 na kuwa ukanda wa kijani.

"Eneo hilo lilitengwa toka enzi za wakati ule Jiji lilipokuwa likifahamika kama Ustawishaji wa Mkao Makuu Dodoma (CDA), na hati miliki ya eneo hilo tayari tunayo, hivyo Halmashauri ya Jiji inawapa notisi ya siku 14 muwe mmebomoa nyumba zenu wenyewe kwa gharama zetu, wanaolima waache mara moja na waliouza maeneo hayo wawarudishie fedha waliowauzia.

"Tangazo la kuwataka mwondoke lilishatolewa kwenu kwa muda mrefu, ninawaomba msibishane na serikali kwa kuwa ni eneo lake, ninawataka mkavunje wenyewe badala ya kusubiri kubomolewa kwa nguvu, ninatoa siku 14 muwe mmetoka wenyewe na mkikaidi tutakuja kuwaondoa wenyewe," alisisitiza Kayombo.

Alisema changamoto hiyo iliyopo kwenye maeneo mengi ambayo Jiji huvamia na wananchi na kuanza kujenga na wengine wakijifanya kama sehemu hizo ni za mababu zao suala ambalo ni hatari kama ilivyo kwa wakazi wa Chikowa ambao wamevamia na kuanza kujenga na kulima mazao ya chakula na biashara.

Baadhi ya wakazi wa mtaa huo wakizungumza kwa nyakati tofauti kwenye kikao hicho, walisema eneo hilo lilikuwa la mababu na bibi zao.

Walisema kutokana na eneo hilo kuwa pori, wameamua kuishi kwa kujenga nyumba na kufanya shughuli kijamii ikiwamo kilimo.

Katibu wa Kamati ya ufuatiliaji wa eneo hilo, Simon Ezekiel, alisema hawako tayari kubomoa nyumba zao na kuacha kulima kwenye eneo hilo kwa siku hizo kwa sababu hawajui pakwenda.

Mzee Stevin Mjelwa, alisema pamoja na wananchi kupenda maendeleo, bado kuna uzembe miongoni mwa watumishi wa Halmashauri na Ofisi ya Mkuu wa wilaya kwa kusababisha mvutano kutokana na tabia yao ya kukaa ofisini badala ya kutembelea maeneo yaliyo wazi kwa miaka mingi.

"Kutowajibika kwa maofisa hao kumesababisha migogoro mingi kujitokeza ndani ya Jiji kati yao na wananchi. Na kwa jinsi hii watu wanaweza kuichukia serikali kutokana na uzembe wao," alisema Mjelwa.

Diwani wa Kata ya Ipagala, Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Gombo Dotto, akiwasisitiza waumini wa Kanisa la International Evangelism Sinai Ipagala Dodoma kwenye ibada ya kuchangia ujenzi iliyofanyika juzi, kujitokeza kuhakiki majina na taarifa zao kwenye daftari la kudumu la wapigakura ili waweze kutambuliwa na kushiriki katika uchaguzi ujao nchini. **PICHA: PETER MKWAVILA**



# Wakala wa vipimo aapa kudhibiti lumbesa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAKALA wa Vipimo (WMA) umesisitiza kuwa utaendelea kuwadhibiti wafanyabiashara wanaotumia lumbesa ili kumfaidisha mkulima na kazi ya mikono yake.

WMA imeahidi kuendelea kufanya ukaguzi wa kushtukiza kila msimu wa mazao ili kuhakikisha mizani zinazotumika zimehakikiwa na wakulima hawaibiwi na baadhi ya wafanyabiashara.

Hayo yalisemwa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Ufundi kutoka (WMA), Albogast Kajungu, katika Maonesho ya Kitaifa ya Kilimo maarufu kama Nanenane yanayoendelea katika Viwanja vya Nzunguni jijini Dodoma.

Kajungu, alisema WMA ina mchango mkubwa katika sekta ya kilimo hususani kwa mazao ya kimkakati ambayo ni korosho, ufuta, kahawa, tumbaku na pamba kuhakikisha suala la vipimo linazingatiwa na wakulima hawaibiwi.

Alisema kazi kubwa ya wakala huo katika sekta hiyo ndogo ya mazao ya kimkakati ni kuhakikisha mizani inayotumika katika ununuzi wa mazao hayo zinahakikiwa ili kujiridhisha kuwa ziko sahihi.

"Lengo ni kuhakikisha kwamba mkulima anapouza mazao yake anapata thamani ya pesa sawasawa na mazao aliyouza," alifafanua Kajungu.

Alisema kazi ya kuhakiki mizani hufanyika kwa awamu mbili, ya kwanza uhakiki wa mizani kabla ya msimu wa kila zao kuanza na ya pili ukaguzi wa kushtukiza.

Alisema wamekuwa wakifanya ukaguzi wa kushtukiza wakati wa msimu kwa kila zao ili kujiridhisha kama vipimo vilivyohakikiwa awali vinatumika kwa usahihi.

"Kwa hiyo kabla ya msimu tunapita kuhakiki mizani zote zinazotumika kununulia mazao na wakati wa msimu tunapita kujiridhisha kama zinatumika kwa usahihi," alisema.

Kwa mujibu wa Kajungu, WMA hutoa elimu kwa wakulima na wananchi ili wafahamu mizani ya kununulia mazao iliyohakikiwa.

Alitaja mojawapo ya sifa za mizani iliyohakikiwa kuwa ni uwepo wa stika ya WMA inayoonesha tarehe ambayo mizani ilihakikiwa pamoja na tarehe ya mwisho ambayo stika hiyo itakuwa imekoma matumizi yake.

"Kwa hiyo mwananchi akiiona ile stika inampa uhakika kuwa mizani hiyo imehakikiwa na WMA," alisisitiza Kajungu.

Kuhusu ufungashaji wa mazao ya shamba, alieleza kuwa kwa mujibu wa sheria, kwa uzito unaozidi kilo 100 unatafsiriwa kama lumbesa ambayo ni kosa kisheria.

Kajungu ametoa wito kwa wakulima na wananchi kufahamu mazao ya shamba lazima yafungashwe kwa uzito unaokubalika kisheria ambao ni kilo 100.

Alisisitiza umuhimu wa kuwepo vituo vya kununulia mazao ambavyo ni rahisi kuweka mizani iliyohakikiwa na WMA ili itumike kwa wakulima.

Alisema hatua hiyo itasaidia kujiridhisha kwamba yamefungashwa katika uzito wa kilo 100 ili kupata faida kwa muuzaji na mnunuzi.





## Wadau waombwa kuzisaidia taasisi za msaada wa kisheria

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WADAU wameombwa kuzisaidia taasisi zinazojishughulisha na utoaji wa msaada wa kisheria kwa wananchi ili ziweze kuwafikia wahitaji wengi wanaoshindwa kupata haki.

Inaelezwa kuwa, kutokana na taasisi zinazotoa msaada wa kisheria kufanya kazi kwa kujitolea, nyingi zinashindwa kuwafikia wahitaji kutokana na kukosa rasilimali fedha na vitendea kazi.

Mkurugenzi wa Shirika la Mbeya Paralegal Aid Centre (MBEPACE), Laiki Ndagile aliyasema hayo alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu mchango wa taasisi za msaada wa kisheria katika upatikanaji wa haki nchini.

Miongoni mwa maeneo aliyoyataja yenye uhitaji wa msaada wa kisheria ni taasisi za elimu zikiwamo shule kwani zinakabiliwa na vitendo vya ukatili kwa watoto lakini matukio hayaripotiwi wala kushughulikiwa kisheria.

Alisema kutoripotiwa na kutokuchukuliwa hatua za kisheria kwa watu wanaofanya ukatili kwenye shule kunatokana na uelewa mdogo wa masuala ya kisheria kwa wanajamii kwenye mambo husika.

"Tumeona shule nyingi sana watoto wanafanyiwa ukatili, na hizo ni chache ambazo zimeripotiwa kwenye mamlaka husika lakini zipo taarifa nyingi sana za ukatili dhidi ya watoto ambazo zimebainika na kuachwa pasipo kutolewa taarifa," alisema Ndagile na kuongeza:

"Wasaidizi wa kisheria tunafanya kazi kwa kujitolea, tunaona taasisi nyingi zinasaidia watu katika maeneo tofauti na wakitokea watu wa kutusaidia kwenye masuala ya kisheria ndani ya jamii tutaifikia jamii kwa upana zaidi," aliongeza.

Alisema iwapo taasisi hizo zitawezeshwa na wadau mbalimbali kutoka kwenye jamii kutarahisiha kuwafikia wanajamii wengi na kutoa huduma kwa upana zaidi, hivyo ni hatua itakayoleta ustawi wa haki na usawa kwa wananchi wa maeneo yote.

# Wakulima watakiwa kuzingatia matumizi sahihi ya pembejeo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wametakiwa kuzingatia matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo ili kuepuka uharibifu wa mazingira na kuifanya sekta hiyo kuwa endelevu.

Kaimu Meneja wa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Josiah Murunya alitoa rai hiyo juzi alipozungumza na Nipashe kwenye maonesho ya wakulima (Nane nane) yanayofanyika katika Uwanja wa John Mwakangale jijini Mbeya.

Alisema ni muhimu wakulima kuzingatia taratibu na kanuni za utunzaji na uhifadhi wa mazingira wanapotekeleza shughuli zao. Akidai kuwa, shughuli hizo ni miongoni mwa shughuli zinazochangia uchafuzi wa mazingira zikifanywa bila kuzingatia taratibu nzuri.

Murunya alisema kilimo ni moja ya shughuli ambazo zinatumia kemikali mbalimbali ikiwamo mbolea na viuatilifu ambavyo visipotumika ama kuhifadhiwa vizuri vinaweza vikachafua mazingira na kukifanya kilimo kutokuwa endelevu.

"Ili kilimo kiwe endelevu ni muhimu kutunza na kuhifadhi mazingira. Aidha, sasa hivi dunia inakabiliwa na tatizo la mabadiliko ya tabianchi ambayo moja ya visababishi ni kilimo kisichozingatia matumizi sahihi ya pembejeo, kwa hiyo niwasihi wakulima kuzingatia matumizi sahihi ya vitu hivi ili kupunguza athari kwenye mazingira," alisema Murunya.

Alisema kwenye maonyesho hayo wapo maofisa mbalimbali wa NEMC ambao wanatoa elimu kwa wananchi hasa wanaojishughulisha na kilimo, ufugaji na uvuvi kuhusu utunzaji na uhifadhi wa mazingira.

Hivyo, alitoa wito kwa wananchi kutembelea ofisi za mamlaka hiyo ili kupata elimu ya mazingira na namna ya kufanya shughuli za maendeleo zinazohifadhi na kulinda mazingira.

"Pia tunatoa elimu ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA) kwa wawekezaji mbalimbali wakiwamo wakulima ili kuwa na uwekezaji bora na kuepukana na tatizo la athari za mazingira endapo akifanya shughuli hizi bila kufanyiwa tathmini ya athari kwa mazingira," alisema Murunya.

Vilevile, alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu katazo la mifuko ya plastiki ambazo ni kelele zinazozidi viwango na kupokea kero za masuala ya mazingira kutoka kwa wananchi mbalimbali na kuzifanyia kazi.

Akifungua maonyesho hayo mwishoni mwa wiki, Naibu Waziri Mkuu, Dk. Dotto Biteko alizitaka taasisi mbalimbali za serikali zinazohusika na kilimo, mifugo na uvuvi kutoa elimu kwa wadau kuhusu utunzaji wa mazingira.

Alisema ili kilimo kiwe endelevu ni muhimu wakulima wakafundishwa mbinu za kisasa ambazo zitawafanya wazalishe bila kuharibu mazingira ikiwamo kilimo hifadhi.




Ofisa wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Emilyo Mwakalobo (kushoto), akimhudumia mwanachama wa mfuko huo aliyetembelea Maonesho ya Wakulima Nanenane Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yanayofanyika katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAKUKURU yanusa ufisadi miradi ya bil.3/- Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MIRADI ya maendeleo tisa yenye thamani ya zaidi ya bilioni tatu iliyochunguzwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Njombe imebainika kuwa na dosari.

Miradi hiyo, ni kati ya miradi 23 ya maendeleo iliyochunguzwa na taasisi hiyo katika wilaya zote za mkoa huo.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Njombe, Kassimu Ephraem, aliyasema hayo juzi wakati akitoa taarifa ya utendaji kazi wa taasisi hiyo katika kipindi cha miezi mitatu kwa waandishi wa habari.

Alisema miradi hiyo 23 iliyochunguzwa ipo katika sekta za elimu, barabara, afya, maji na ujenzi wa nyumba za watumishi ambazo gharama yake ni zaidi ya Sh. bilioni 8.76.

Alisema baada ya kubaini upungufu katika miradi hiyo tisa tayari wametoa maelekezo mbalimbali ili kuirekebisha na iweze kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi.

Alisema wanaendelea kuwakumbusha makandarasi, wazabuni, wahandisi, mafundi, wanakamati na wasimamizi wa miradi ya serikali kutimiza wajibu wao kwa weledi na uaminifu ikiwa ni sambamba na utunzaji wa nyaraka zinazohusiana na matumizi ya fedha.

Pia alisema wamejipanga kudhibiti vitendo vya rushwa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na wananchi, vyama vya siasa na wadau.

"Natoa rai kwa wananchi wote kutoa taarifa kwetu sisi pale wanapoona viashiria vyovyote vya rushwa katika maeneo yao wakati wa mchakato wa kuwapata viongozi watakaogombea," alisema Ephraem.

Alisema TAKUKURU imejiwekea mikakati ya kuhakikisha kwa kipindi cha Julai hadi Septemba mwaka huu kutoa elimu kwa jamii kuhusu athari za vitendo vya rushwa na namna ya kushiriki katika kuzuia vitendo hivyo visitokee.

Aidha, kwa upande wa mashtaka, Ephraem alisema mashauri matatu yanaendelea mahakamani na mashauri manne yametolewa hukumu, mashauri mapya yakiwa mawili na mashauri yalioshinda ni mawili.

Aidha, baadhi ya wananchi mjini Njombe, akiwamo Jarome Mgaya alisema taasisi hiyo inapaswa kuendelea kutoa elimu hasa kwa watumishi wa serikali kwa sababu pindi viongozi wa kitaifa wanapokuja huwa wanabaini upungufu katika miradi lakini hakuna hatua zinazochukuliwa.

"Unakuta kiongozi mkubwa amekuja na kukagua mradi na kubaini ubadhirifu lakini hatuoni hatua zikichukuliwa," alisema Mgaya.





# Mradi uwezeshaji wajasiriamali vijana vijijini wazinduliwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo cha China (CAU), imezindua mradi wa uwezeshaji wa wajasiriamali vijana katika maeneo ya vijijini.

Mradi huo unalenga kuwekeza katika ujuzi na welezi wa vijana kutumia fursa zilizopo vijijini na kukuza uchumi.

Akizungumza jana katika hafla hiyo visiwani Zanzibar, Waziri wa wizara hiyo, Omar Said Shabani, alisema maeneo ya vijijini kuna fursa nyingi hazijatumiwa kwa sababu vijana hawana mwamko wa kuzitumia fursa hizo katika shughuli za kimaendeleo.

Alisema mradi huo utaanza na vijana 15 kupatiwa mafunzo ya ujasiriamali nchini China, ambapo kati ya hao, 10 kutoka nchini Uganda na watano kutoka Zanzibar.

Hivyo, aliwataka vijana hao kwenda kujifunza kwa sababu China imeendeleza zaidi katika maendeleo ya vijana.

Alisema China hutumia rasilimali zinazopatikana nchini mwao hasa katika kuongeza thamani, hivyo vijana hao watakuwa mabalozi wazuri kwa vijana wenzao katika kuchangia shughuli za maendeleo.

"Mpango huu, unaoongozwa na Chuo Kikuu cha Kilimo cha China kwa kushirikiana na Shirika la Thamani Endelevu la Jamii la Tencent, ni ushahidi wa nguvu ya ushirikiano wa kimataifa katika kuendesha mabadiliko ya maana ya kujenga jamii," alisema.

Aidha, alisema mpango huo utaongeza uzalishaji wa kilimo, kukuza mazoea endelevu na hatimaye kuchangia ustawi wa kiuchumi wa Zanzibar.

Naye Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Fatma Khamis, alisema kwa kutumia utaalamu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha China, utawawezesha wajasiriamali wadogo kustawi katika soko la ushindani la kimataifa.

Alisema mpango huo hutoa rasilimali muhimu kama vile mbegu bora, vifaa vya kisasa vya kilimo, zana za kiteknolojia.

Mwenyekiti wa chuo hicho, Professa Li Xiaoyun, alisema Zanzibar ni maarufu sana kwa kilimo cha viungo, hivyo ni sehemu nzuri katika kusaidia maendeleo ya vijana na kukuza uchumi wa nchi.

Akizungumza kwa niaba ya wajasiriamali wezake, Makame Chumu Shaali, alisema fursa hiyo ni muhimu kwao hasa katika ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia na itawapa nafasi ya kujifunza uchumi wa Zanzibar hasa katika upande wa vijijini.

Alisema pia itamwongezea taaluma katika elimu na kuwa mahiri katika uchumi wa buluu na kilimo hasa ikizingatiwa kuwa China imeendelea katika sekta ya kilimo.




Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda wa Zanzibar, Omar Said Shaban (kulia), akisalimiana na Meneja Mkuu wa Asasi ya NMB Foundation, Nelson Karumuna (katikati), wakati wa hafla ya uzinduzi wa mafunzo kwa wakulima wa mwani yalioratibiwa na asasi hiyo kwa ushirikiano wa Benki ya NMB na kampuni ya Mwani Zanzibar (ZASCO). Kushoto ni Mkuu wa Idara ya Kilimo Biashara wa NMB, Nsolo Mlozi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Rushwa, ufisadi katika miradi yaiibua ACT-Wazalendo

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kuwa hakuna nchi inayoweza kupiga hatua ya maendeleo bila ya kudhibiti vitendo vya rushwa na ufisadi hasa katika miradi ya maendeleo.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Ismail Jussa Ladhu, alisema hayo jana wakati akihutubia mkutano wa hadhara, uliofanyika Uwanja wa Kwageji Mkoa wa Mjini Magharib Unguja.

Jussa alisema miradi mingi ya ujenzi Zanzibar inakabiliwa na tatizo la ufisadi na ndiyo chimbuko la kusuasua kwa mradi wa ujenzi wa Barabara ya Chakechake hadi Wete inayofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Kiarabu (BADEA) na Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (Saund Fund).

"Unaweza kujiuliza kwanini kila mkutano mimi nimeshika ajenda ya kuelezea wizi na ufisadi, kwa sababu hakuna nchi itakayosonga mbele ikiwa inaendeshwa na wizi na ufisadi," alisema Jussa.

Aidha alisema serikali inapaswa kupambana na vitendo vya rushwa kupitia miradi ya ujenzi kwa vile gharama za vifaa vya ujenzi haifanani na bei halisi katika soko la kawaida na ile ambayo inanunuliwa katika miradi ya ujenzi.

Alisema hali hiyo inaonyesha wazi kuwa kuna ufisadi wa kutisha hasa katika ununuzi wa vifaa vya ujenzi ikiwamo nondo na saruji.

Akizungumzia mradi wa ujenzi wa Barabara ya Chakechake hadi Wete, alisema mradi huo unaendelea kudorora kutokana na kupigwa vita na baadhi ya viongozi ambao hawataki kampuni ya Mecco kuendelea na ujenzi wa mradi huo.

Alisema pamoja na wafadhili kupinga kitendo cha Mecco kutaka kunyang'anywa kazi na serikali bado wameendelea kuwekewa vikwazo, ikiwamo wananchi kutolipwa kwa wakati ili kupisha mradi wa ujenzi huo, jambo ambalo limechangia kuchelewa ujenzi wa barabara hiyo.

Alisema mpaka sasa wananchi kuanzia Limbani hadi Wete bado hawajalipwa fidia na fedha za maendeleo ya ujenzi haziwasilishwi kwa wakati na serikali licha ya mshauri elekezi wa mradi kupewa barua za maombi kwa wakati.

Mradi wa ujenzi wa barabara ya kilomita 22 kutoka Chakechake hadi Wete Pemba unatarajia kutumia Euro 457, ulianza mpango wake tangu uongozi wa Rais Mstaafu Amani Abeid Karume.

Mwenyekiti wa chama hicho, Othman Masoud Othman, alisema ni hatari kwa serikali kuchukua mikopo yenye thamani kubwa zaidi kuliko Bajeti Kuu ya Serikali ambayo ni Sh. trilioni 1.5 kutokana na uchumi mdogo wa Zanzibar. Alisema mpaka sasa serikali imekopa Sh. trilioni tatu katika kipindi cha miaka minne, kiwango ambacho ni kikubwa ikilinganishwa na hali halisi ya uchumi wa Zanzibar.

Akizungumzia suala la uchaguzi, Othman alisema chaguzi za Zanzibar zimekuwa na matatizo kutokana na misingi ya demokrasia na utawala bora kutozingatiwa na kusababisha watu kupoteza maisha na wengine kupata ulemavu wa kudumu.

# Wanaume wanaonyonya matiti ya wanawake waonywa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, ametoa onyo kwa wanaume wanaonyonya matiti ya wanawake wenye watoto wachanga, akiwataka kuacha tabia hiyo.

Badala yake amesema watoto ndiyo wanaostahili kunyonya matiti hayo kwa ajili ya kuwa na afya nzuri.

Alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisi kwake kuhusu wiki ya unyonyeshaji, akisema takwimu za mwaka 2022 za unyonyeshaji wa matiti ya mama pekee katika kipindi cha miezi sita kwa Zanzibar ni asilimia 41.

Alisema hali hiyo inayoonyesha kwamba bado kuna kundi kubwa la watoto wanaolishwa mapema.

Mazrui alisema unyonyeshaji watoto matiti ya mama pekee humsaidia mama kurudia hali yake ya uzito wa kawaida sawa na uzito aliokuwa nao kabla ya ujauzito.

Waziri huyo alisema unyonyeshaji wa matiti ya mama ni uamuzi sahihi ambao hauathiriwa na mazingira na husaidia katika uhakika wa chakula hata katika nyakati za majanga, hivyo kulinda, kuhamasisha na kusaidia wanawake katika unyonyeshaji ni muhimu kwa afya ya mama na mtoto.

Aidha, alisema unyonyeshaji wa matiti ya mama una faida nyingi zikiwamo, humpatia mtoto kinga dhidi ya maradhi mbalimbali kama kuharisha magonjwa ya utapiamlo na magonjwa ya njia ya hewa.

Alisema pia huleta uhusiano mzuri na wa karibu kati ya mama na mtoto, humwezesha mtoto kukua vizuri kiakili na kimwili na kuwa na afya njema.

Alisema pia hupunguza uwezekano wa mama kupata ujauzito katika miezi sita ya mwanzo, hupunguza uwezekano wa mama kupata saratani ya kizazi.

Mazrui alisema pamoja na kuwa unyonyeshaji ni msingi wa maendeleo ya afya ya mtoto, vilevile ni msingi wa maendeleo ya nchi kwa kiwango kikubwa unyonyeshaji unasaidia kuondoa mzunguko wa umasikini.


"Hivyo basi nguvu za pamoja zinahitajika kuhakikisha unyonyeshaji unafanyika, kwa kushirikiana wadau mbalimbali katika kulinda, kuhamasisha na kusaidia haki za wanawake kunyonyesha mahala popote na muda wowote," alisema.

"Wiki ya Unyonyeshaji huadhimishwa kila mwaka ifikapo tarehe 1-7 ya mwezi wa nane. Kauli mbiu ya mwaka huu ni: "Ondoa Vikwazo (changamoto) saidia unyonyeshaji wa maziwa ya mama pekee katika kipindi cha miezi sita," alisema.

Kiongozi kutoka Shirika la Kimataifa la kuwahudumia Watoto (UNICEF), Zanzibar, Lax Mi, alisema takwimu za unyonyeshaji zinaendelea kuimarika ingawa kazi zaidi inahitajika.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**BRIAN ZEDEKIA MANGI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1619-0077** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **VICTORY SECONDARY SCHOOL** mwaka 2020. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/TEM/162729/2024**

---

**REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT 334 R: E 2019**
**CHANGE OF NAME BY DEED POLL.**

**THIS CHANGE OF NAME DEED** is made this 30th day of July 2024 by me **STEPHANO CHARLES DAUDI** formerly known as **STEVE CHERLES DAUDI** a resident of Arusha .

**WITNESSES AND IT IS HEREBY DECLARED a**s follows:

1. I absolutely renounce and abandon the use of my said former names of **STEVE CHERLES DAUDI** and I assume and determine to take and use the new name of **STEPHANO CHARLES DAUDI** in substitution of my former names of **STEVE CHERLES DAUDI .**
2. **REASONS** for such change of name is due to I, want to change the name appeared on my National ID no. **19980505-23210-00004-27** which is not a correct name of mine and using the name appeared on my Academic certificates as aforesaid .
3. **I DECLARE** I shall at all times hereafter in all records, documents and other writings and in all actions and dealings and on all occasions whatsoever use the new name of **STEPHANO CHARLES DAUDI** in substitution for my former names of **STEVE CHERLES DAUDI** so relinquished as aforesaid to the intent that I may hereafter be known not by aforesaid former names, but by the new name only.
4. **AND I HEREBY AUTHORISE AND REQUIRE** all persons at all times to describe and address me by the new name of **STEPHANO CHARLES DAUDI**

IN WITNESS whereof I have hereunto subscribed my new name of **STEPHANO CHARLES DAUDI ,** and have affixed my signature the day and year herein written.

SIGNED and DELIVERED by the said STEPHANO CHARLES DAUDI who is known to me personally, in my presence this 30th day of July 2024. ............ DEPONENT



BEFORE ME:
Name: JACOB V. MALICK
Address: 11444, ARUSHA
Signature: ............
NOTARY PUBLIC &COMMISSIONER FOR OATHS

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**REGISTRATION OF DOCUMENT ACT**
**Made under CAP 117 (RE:20021)**
**CHANGE OF NAME BY DEED POLL.**

**BY THIS DEED, I MEDICA GERVAS BALENGE** residence of Arusha Region, my name has been mistakenly written as **MDECA GERVAS SHARABU** on my bank account, I absolutely renounce and abandon the said names of **MDECA GERVAS SHARABU** in lieu thereof assume and adopt as from the date hereof, the names of **MEDICA GERVAS BALENGE .**

**AND**

**IN PURSUANCE** of such changes of names aforesaid, **I HEREBY DECLARE THAT, I** shall at all times in all records ,deeds transactions, proceedings. dealings **MEDICA GERVAS BALENGE**,in writing and upon all occasions whatsoever use and sign the said names of **MEDICA GERVAS BALENGE** as my names in lieu of the said names of renounced as aforesaid.

**AND**

**I HEREBY AUTHORISE** and request all persons to designate and address me in the names of **MEDICA GERVAS BALENGE.**

**HENCE**

**I, MEDICA GERVAS BALENGE** make this declaration conscientiously believing the same to be true and in accordance with the provisions of the Oaths and statutory declaration **ACT.CAP,34 (RE:2002).**

**IN WITNESS WHEREFORE** I have hereunto, subscribed the names of on the **DAY** and the **MANNER** hereinafter appearing.

**AFFIRMED** and **DELIVERED** at Arusha by the Said **MEDICA GERVAS BALENGE** who is known to me personally /Introduced to Me by........................the later being Known to me personally in my presence This 15th day of March 2024. ............ DEPONENT



BEFORE ME:
NAME: Maisara Kassim
SIGNATURE: ............
ADDRESS: 7091 Arusha
OCCUPATION: COMMISSIONER FOR OATHS

---

## KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA

**AZZA SAID RASHID** anatangaza kupotea kwa offa ya kiwanja namba 11 kitalu AIII kirumba manispaa ya ilemela Mwanza yenye jina la mmiliki aliyeandikishwa **TAUSI MTORO** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu

TAARIFA YA POLISI:
**PHQ/SHI/SHI/197/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ENOCK AGUSTINO MWALONGO** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba **MC 980 CFY.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochte cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**PHQ/MBE/MBE/13830/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI.

**OSCAR MATEI MHANILA,** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 488 BGD** kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi

TAARIFA YA POLISI:
**PHQ /RUV/MBI/4610/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JOSEPH EGNO KOMBA** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili MC 250 CEC aina ya HONLG kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi:

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MAULID NDINGE MKENDA,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari aina ya **Toyota Prado** yenye namba za usajili **T.393 EHM,** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

TAARIFA YA POLISI:
**PHQ/DOD/DOD/33254/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ABSALOM GWANKIPYA MWAFYELA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T 169 CYL.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**PHQ/MBE/RUN/22300/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**AMANI NODI MWANI** Anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye jina la umiliki **GS GROUP LIMITED** usajili namba **MC 508 DTW** Chassis namba **LC6PCJK27NOA66898.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**PHQ/RUV/4577/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ERICK ALPHONCE MAPUNDA** Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye jina la umiliki **DIOCESE OF SONGEA** yenye usajili namba **T280 DRF** Chassis namba **JTEEV73J500007882.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SIMON CHISOTE SILWIMBA** Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **ISUZU BIGHORN** yenye usajili namba ***T278 BER*** Chassis namba **UBS69GW8152087.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**THOMAS VILIGINI MBILINYI** Anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye jina la umiliki **GS GROUP LIMITED** yenye usajili namba **MC 899 DXZ** Chassis namba **LC6PCJK21P0037896.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**PHQ/RUV/SON/3994/2024**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha DODOMA MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na.53/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ATHUR DOMINIC CHUNDU wa BAHI ROAD**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MARY CHUNDU NKOSWE**

**TANGAZO**
**(Kanuniya 5(2) ya Kanuniza Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 21 Mwezi 08 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 31 Mwezi 07 Mwaka 2024.

HAKIMU
PRINCIPAL PRIMARY COURT MAGISTRATE
URBAN DODOMA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA WILAYA SINGIDA**
**(TAARIFA YA KUSIKILIZWA SHAURI)**

**SHAURI LA RUFAA/ MAOMBI/ MADAI NA 13990 MWAKA 2024**

**MPEMBA FEA ................................MWOMBA RUFAA**

**DHIDI YA**

**DIGA MASUNGA..................................MJIBU RUFAA**

**Wito kwa DIGA MASUNGA WA MOROGORO**

Fahamu kwamba tarehe 6/8/2024 saa: 8:30 asubuhi ndio siku ya kusikilizwa shauri la rufaa/ maombi
Fahamu kwamba ikiwa Hautahudhuria kama unavyoamriwa kupitia wito Huu Bila Sababu ya Msingi, utashtakiwa kwa kosa la kudharau au kupuuza amri Halali ya mahakama.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe 18/7/2024
Nmekubali kupokea, kuitwa shaurini;

HAKIMU

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 16634 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late JACKSON NATHANIEL KOBELO of Dodoma Within Dodoma City.**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY REHEMA JACKSON KOBELO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 05 Day of 9, 2024

Date at Dodoma this 02 Day of 08, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA DISTRICT

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# 100 wafariki maandamano Bangladesh

**DHAKA,** Bangladesh

TAKRIBANI watu 100 wameuawa na mamia kujeruhiwa wakati wimbi jipya la maandamano dhidi ya serikali likizidi kuenea kote nchini Bangladesh.

Waandamanaji wanamshinikiza Waziri Mkuu, Sheikh Hasina, ajiuzulu huku kiongozi huyo akiwashutumu waandamanaji kwa hujuma za kukata mawasiliano ya simu kwa nia ya kuzima machafuko.

Vyombo vya habari nchini humo vilisema takriban watu 95, wakiwamo maofisa wa polisi 14, walikufa katika ghasia hizo. Huku kituo kingine cha habari cha Channel 24 kikiripoti vifo vya watu wasiopungua 85.

Jeshi lilitangaza kuwa amri mpya ya kutotoka nje imeanza kutumika Jumapili jioni kwa muda usiojulikana, ikijumuisha katika mji mkuu wa Dhaka na makao makuu mengine ya tarafa na wilaya.

Ilielezwa kuwa awali serikali ilikuwa imeweka amri ya kutotoka nje isipokuwa baadhi ya maeneo ya Dhaka na kwingineko.

Waandamanaji wanamtaka Waziri Mkuu Hasina ajiuzulu kufuatia maandamano ya mwezi uliopita yaliyoanzishwa na wanafunzi wakitaka kusitishwa kwa mfumo wa ajira serikalini wanaodai ulikuwa na upendeleo.

Maandamano hayo yalizidi kuwa ya ghasia na kusababisha vifo vya zaidi ya watu 200.

Wakati vurugu hizo zikiendelea, Hasina alisema waandamanaji walioshiriki katika hujuma na uharibifu hawakuwa wanafunzi tena bali ni wahalifu, na kuongeza kuwa watu wanapaswa kushughulikia kwa mikono ya chuma.

Chama Tawala cha Awami League kilisema shinikizo la kumtaka Hasina kujiuzulu, linaonyesha kuwa maandamano hayo tayari yametekwa na chama kikuu cha upinzani cha Bangladesh Nationalist Party na chama ambacho sasa kimepigwa marufuku cha Jamaat-e- Islami.

Serikali pia imetangaza mapumziko ya umma ya siku tatu kuanzia jana Jumatatu hadi Jumatano. Na kwamba mahakama zitapaswa kufungwa kwa muda usiojulikana.

Huduma ya mawasiliano ya simu huku mitandao ya kijamii ya Facebook na mingine ikiwa ni pamoja na WhatsApp, pia imezimwa.

Takriban watu elfu 11,000 wamekamatwa katika wiki za hivi karibuni. Machafuko hayo pia yamesababisha kufungwa kwa shule na vyuo vikuu kote nchini.

Mkuu wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa, Volker Turk, alisema ghasia za kutisha nchini Bangladesh lazima zikomeshwe na kuelezea wasiwasi wake kuhusu vifo zaidi kabla ya maandamano makubwa huko Dhaka.

Aidha, mkuu huyo aliitaka serikali nchini humo kuacha kuwalenga waandamanaji katika maandamano ya amani. **DW**

**Takriban watu elfu 11,000 wamekamatwa katika wiki za hivi karibuni. Machafuko hayo pia yamesababisha kufungwa kwa shule na vyuo vikuu kote nchini.**



Waandamanaji Bangladesh wakiuzunguka moto katika maandamano ya kuipinga serikali. **PICHA: MTANDAO**

## WHO kutathimini maambukizi ya mpox

**GENEVA,** Uswisi

MKURUGENZI Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) ,Tedros Ghebreyesus, amesema anatathimini kukutana na kamati maalum, kuamua iwapo maambukizo ya ugonjwa wa mpox unaosambaa barani Afrika unapaswa kutangazwa kama janga la kimataifa.

Kauli hii ya Ghebreyesus inakuja wakati huu mataifa mbalimbali yakianza kuchukua tahadhari kuzuia kusambaa kwa maambukizi hayo, ambayo tangu mwezi Septemba mwaka uliopita, yamekuwa yakisambaa kwa kasi nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Kufikia Julai 11, mwaka huu, WHO ilisema maambukizi 11,000 yalikuwa yameripotiwa DRC na kusababisha vifo 445 mwaka huu pekee, watoto wakiwa waathiriwa wakubwa.



Wiki iliyopita, Umoja wa Afrika ulisema unahitaji kwa haraka Dola Milioni 10.4 kuunga mkono taasisi yake ya afya Africa CDC kuzuia kusambaa kwa ugonjwa huo kwa kuongeza kasi ya vipimo na kutafuta chanjo.

Mwezi uliopita, Burundi iliripoti maambukizi matatu, huku kesi ikiripoti kisa kimoja kutoka kwa abiria aliyekuwa ametokea Uganda.

Jumamosi iliyopita, Uganda nayo iliripoti visa viwili vya mpox ikisema walioambukizwa walitokea nchini DRC. **RFI**

## Nchi za Afrika zaonyesha wasiwasi kuhusu ICC

**HAGUE,** Netherland

WACHAMBUZI wa masuala ya siasa na kimataifa wameonyesha wasiwasi wao kuhusu Mahakama ya Uhalifu ya Kimataifa (ICC) wakihoji malengo ya mahakama hiyo, huku wakijiuliza maswali juu ya upendeleo unaoonekana dhidi ya mataifa ya Afrika.

Pia wanahoji kuhusu athari zake kwa uhuru wa kitaifa, na madai ya maelekezo ya kisiasa.

Waangalizi wa kimataifa nao wameonyesha mashaka kama nchi za Afrika na zile za Kusini mwa dunia kuwa kweli zinafaidika na taasisi hiyo ambayo msingi wake unaonekana kufanya haki kwa kuchagua, kuzitolea macho nchi za Afrika, na kuacha mataifa yenye nguvu kukwepa uwajibikaji.

Ilielezwa kuwa zaidi ya miongo miwili iliyopita wakati ilipoanzishwa jijini Roma, ICC ilileta matumaini kwa ajili ya siku zijazo za sheria za kimataifa kwa kuwa wengi walidhani ingekuwa kiongozi wa kesi za uhalifu wa kivita.

Nchi zote za Amerika Kusini na idadi kubwa ya nchi za Afrika zilisaini mkataba wa Roma unaoanzisha ICC, wakiwa na imani na malengo ya kimsingi kwamba ICC itawafikisha wahalifu wa ukatili wa kivita, mauaji ya kimbari, na uhalifu dhidi ya ubinadamu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Haki za Kimataifa (GJC), Elise Keppler, alisema ndoto kuu ilikuwa kwamba ICC itatoa haki kwa waathiriwa.

Alisema Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lilianzisha mahakama mbili zenye lengo la kuhukumu uhalifu uliofanyika Rwanda na Yugoslavia ya zamani.

Viongozi 120 waliokutana Roma, Italia walikubali kuanzishwa kwa ICC ili kuchukua nafasi za mahakama hizo za muda.

Wakati wa maadhimisho ya ICC, Julai, 17 mwaka huu, Rais wa ICC, Jaji Tomoko Akane aliliambia jopo katika makao makuu ya Umoja wa Mataifa (UN) New York kwamba. "Mwongozo wetu pekee ni sheria inayohusika, ambayo kwanza na muhimu ni mkataba wa Roma, uliotungwa kulinda ubinadamu. Kila mtu ni sawa mbele ya sheria na hakuna mtu aliye juu ya sheria."

Mshauri wa kisheria kuhusu haki za kibinadamu na sheria za kimataifa kutoka Shirika la Amnesty International, Melissa Hendrickse, alisema rasimu za kuzuia na kutoa hukumu dhidi ya uhalifu wa binadamu ziliandaliwa na Tume ya Sheria za Kimataifa (ILC) kati ya mwaka 2013 na 2019. **DW**

# AZAM FC YAFUATA NYAYO ZA YANGA

Na Adam Fungamwango

TIMU ya Azam FC imefanikiwa kupata taji la kwanza msimu huu kabla ya kuanza kwa michuano ya Ngao ya Jamii, Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA, kama ilivyokuwa kwa Yanga.

Kikosi cha Azam kiliwasili nchini alfajiri ya jana kikitokea Kigali nchini Rwanda ambako kilicheza mechi maalum dhidi ya Rayon Sport na kupata ushindi wa bao 1-0 lililowekwa ndani ya wavu na Lusajo Mwaikenda.

**Mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa Pele, Kigali ilikuwa ni maalum kwa tamasha kwa timu zote mbili kutambulisha wachezaji wao wapya wamsimu, Azam wakiita Azamka, na wenyeji wao wakiita,' Rayon Sports Day.'**



Kabla ya mechi hiyo, timu zote zilitambulisha wachezaji wake wote ambao itawatumia kwa msimu ujao wa mashindano.

Kombe la Choplife ambalo wamelichukulia Rwanda, limekuwa la kwanza kwa Azam kama ilivyokuwa kwa Yanga ambao walitwaa Kombe la Toyota nchini Afrika Kusini kwa kuifunga Kaizer Chiefs mabao 4-0. Kwa maana hiyo, Azam na Yanga kila mmoja ana taji moja kabla ya kuanza rasmi msimu wa mashindano.

Kocha Mkuu wa Azam, Youssouph Dabo, ameonesha kufurahishwa na ushindi pamoja na kutwaa taji hilo, hivyo sasa akili yake ameielekeza kwenye mechi ya Ngao ya Jamii dhidi ya Coastal Union.

"Ushindi umetupa faraja kwa sababu umetupatia taji ambalo limetufanya kujiamini, sasa akili na nguvu zote tunazielekeza Alhamisi ijayo katika mechi ya Ngao ya Jamii dhidi ya Coastal, nadhani tutafanya vizuri," alisema.

Mbali na mechi hiyo, Azam pia inajiandaa na mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya APR ya Rwanda, utakaochezwa Agosti 16 au 18, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, na mechi ya marudiano itakuwa Kigali, Agosti 23 au 26.

## Wachezaji Dodoma Jiji kuja kivingine msimu ujao

Na Adam Fungamwango

WACHEZAJI wa Dodoma Jiji wamewaahidi mashabiki wa timu hiyo kuwa watafanya vyema msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, tofauti na msimu uliopita.

Wakizungumza kwenye kambi ya timu hiyo jijini Arusha, wachezaji hao wamesifu maandalizi bora ambayo yamefanywa kuelekea msimu ujao ambao unawapa matumaini ya kutoa ushindani mkubwa na lengo ni kumalizika ndani ya tano bora msimu ujao.

Straika Emmanuel Martin, amesema yupo kwenye kikosi hicho msimu wa nne sasa, lakini safari hii kumekuwa na maandalizi makubwa mno.

"Nipo msimu wa nne sasa, lakini maandalizi ya msimu huu yapo tofauti sana, tupo Arusha sehemu ambayo ina baridi sana, lakini tunapambana nayo na tumeizoea," alisema mchezaji huyo wa zamani wa Yanga.

Kiungo Salmin Hoza aliwaahidi mashabiki kukaa mkao wa kula, lakini akaomba ushirikiano wao kwa kuwaunga mkono kuja viwanjani, hasa Uwanja wa Jamhuri Dodoma ambao ndiyo uwanja wa nyumbani.

"Kwa maandalizi ya msimu huu nadhani tutafanya vyema, ukizingatia kuwa msimu uliopita hatukufanya vyema, hivyo viongozi na wachezaji hatuhitaji tena kumaliza ligi kama msimu uliopita, tumejipanga kufanya vizuri," alisema.

Naye Mohamed Colour, alisema lengo lao msimu ujao ni kumaliza kwenye nafasi tano za juu.

"Matarajio yetu ni kumaliza kwenye kuanzia nafasi ya tano kwenda juu na si vinginevyo," alisema mchezaji huyo.

# Washindi wa mashindano ya Gofu ya KCB East Africa Golf Tour kuwakilisha Tanzania nchini Kenya

Timu iliyoshinda katika KCB East Africa Golf Tour, upande wa Tanzania, imepata fursa ya kushindana katika fainali kuu nchini Kenya tarehe 6 Desemba, ikiwa imedhaminiwa kikamilifu na KCB Bank Tanzania.

Baada ya kumalizika kwa KCB East Africa Golf Tour 2024 nchini Tanzania, hafla ya utoaji tuzo ilifanyika tarehe 3 Agosti 2024 katika Lugalo Golf Club, Dar es salaam. Mbali na fursa ya kushiriki katika fainali kuu, washindi kategori mbalimbali walipokea zawadi.

Washindi wakuu, Peter Mlewi, Meja Jenerali Ibrahim Mhona, Hadija Selemani, na Hawa Wanyeche, walikuwa wachezaji bora wa gofu waliopewa heshima ya kuiwakilisha Tanzania katika fainali kuu nchini Kenya. Ujuzi wao wa kipekee na kujitolea kwao kumehakikisha wanapata malazi kamili na nafasi ya kushindania zawadi kuu ya KES milioni 1, sawa na karibu TZS milioni 20.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, akiwa ameandamana na Afisa Mtendaji Mkuu wa KCB Group, Paul Russo, Mkurugenzi wa Bodi wa KCB Bank Tanzania, Jacqueline Woiso, Mkurugenzi wa Biashara za Kanda wa KCB Group na Mkurugenzi Mtendaji wa KCB Tanzania, pamoja na Mkurugenzi wa Fedha wa KCB Group. Hafla hiyo ilihudhuriwa na wachezaji mashuhuri wa gofu na wateja wa KCB, wakisherehekea mafanikio ya washiriki na maadili ya ubora na michezo yanayochapishwa na KCB Bank.




*Wazirl wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro akizungumza wakati wa hafla ya utoaji zawadi kwa washindi wa mashindano ya mchezo wa gofu ya KCB East Africa Golf Tour 2024 yaliyofanyika katika viwanja vya Lugalo siku ya jumamosi. Washindi wanne wa mashindano hayo wamepata nafasi ya Kwenda kuiwakilisha Tanzania nchini Kenya kwa udhamini wa KCB Bank Tanzania.*

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### MATIP AWINDWA

MLINZI wa zamani wa Liverpool na Cameroon, Joel Matip mwenye umri wa miaka 32 analengwa na Bayer Leverkusen baada ya kuondoka kwa wekundu hao msimu uliopita kwa uhamisho wa bila malipo. ***(Sky Germany)***

#### GOMEZ HATAKI KUONDOKA

BEKI wa England, Joe Gomez hana nia ya kuondoka Liverpool msimu huu, licha ya klabu hiyo kumpa mkataba wa kubadilishana na Newcastle kwa ajili ya winga, Anthony Gordon mwenye umri wa miaka 23. ***(Mirror)***

#### O'RILEY KUMRITHI GALLAGHER

CHELSEA inaweza kumnunua kiungo wa kati wa Celtic raia wa Denmark, Matt O'Riley mwenye umri wa miaka 23 ikiwa kiungo wa kati wa England, Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 24, atajiunga na Atletico Madrid. ***(Sky Sports)***

#### BEIER AWANIWA DORTMUND

KLABU ya Borussia Dortmund inaongoza Chelsea na Aston Villa katika mbio za kuwania kumsajili fowadi wa Hoffenheim, Maximilian Beier mwenye umri wa miaka 21. ***(Sky Germany)***

#### ROYAL ATAKIWA MILAN

AC Milan imewasilisha ombi la thamani ya euro milioni 15 pamoja na nyongeza ili kumsajili beki wa Brazil, Emerson Royal mwenye umri wa miaka 25 kutoka Tottenham Hotspur. ***(Fabrizio Romano)***

#### FULLKRUG SAFI WEST HAM

MSHAMBULIAJI wa Ujerumani, Niclas Fullkrug mwenye umri wa miaka 31, amekamilisha vipimo vyake vya afya kule West Ham kabla ya kuondoka Borussia Dortmund. ***(Sky Sports)***

#### CLACK AULIZIWA

LEEDS United imeuliza kuhusu upatikanaji wa kiungo wa kati wa England, Bobby Clark mwenye umri wa miaka 19 kwa mkopo kutoka Liverpool. ***(Football Insider)***

#### JUVENTUS KUUZA NANE

KLABU ya Juventus inataka kuwaondoa nyota nane katika mabadiliko ya msimu huu, akiwamo fowadi wa Italia, Federico Chiesa mwenye umri wa miaka 26, ambaye amekuwa akihusishwa na Tottenham Hotspur. ***(Mail)***

#### MAN, ARSENAL ZAMTAKA

MANCHESTER United na Arsenal pia zinavutiwa na dili la bei iliyopunguzwa kwa Federico Chiesa, ambaye yuko katika mwaka wa mwisho wa mkataba wake. ***(TeamTalks)***

#### BRANTHWAITE KUUZWA

KLABU ya Everton inaweza kulazimishwa kumuuza mlinzi wa England, Jarrad Branthwaite mwenye umri wa miaka 22, chini ya bei inayotakiwa ili kuepusha matatizo ya kifedha. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Klabu ya Paris Saint-Germain imeripotiwa kuwasilisha ombi rasmi la kutaka kumsajili mshambuliaji wa Manchester City, Julian Alvarez ambaye anawindwa na Atletico Madrid.

**Alvarez anaaminika kutokuwa shwari katika Uwanja wa Etihad kutokana na kukosa nafasi ya kucheza kikosi cha kwanza, baada ya kujikuta akiwa chaguo la pili mbele ya Erling Haaland chini ya Kocha Pep Guardiola.**

Mshambuliaji huyo amekiri wazi hitaji lake la kufikiria chaguo lake msimu huu wa joto lakini hivi majuzi alihamia kupoza uvumi huku Arsenal na Chelsea zikionesha nia ya kumtaka.

### ●●● Yatoa ofa huku mwenyewe akipendelea zaidi kwenda Atletico Madrid...

Hata hivyo, kwa mujibu wa Gaston Edul, nia ya PSG na Atletico inaendelea kukua. Wafaransa hao wanasemekana kuwasilisha ofa rasmi ili kumnasa Alvarez msimu huu wa joto.

Hakuna ada iliyotajwa lakini ofa ya PSG inatarajiwa kuzidi dau lililotolewa na Atletico, ambao wanatayarisha pendekezo la euro milioni 60.

Ofa ya mkataba wa PSG pia inaaminika kuvuka masharti yaliyopendekezwa na Atletico, lakini timu hiyo ya Hispania bado ina faida kwani Alvarez angependelea kucheza Madrid badala ya Paris.

Guardiola aliulizwa kuhusu mustakabali wa Alvarez wakati wa mkutano wake na waandishi wa habari kabla ya mechi ya kirafiki ya kujiandaa na msimu dhidi ya Chelsea Jumamosi.

"Hakuna habari," alisisitiza. "Sina habari yoyote.

"Angalia, Julian anastahili sasa kuchukua muda wake, kile anachohitaji kurejea akiwa safi. Sio tu kwenye miguu - watu wanasema ni miguu.

"Na inahitaji sana, nguvu nyingi, sio kimwili tu, watu hawaelewi. Na ndio maana wanahitaji mapumziko, na ndio maana wanahitaji likizo na hawakuweza kuja hapa. Mashabiki wangependa, ningeipenda, lakini wachezaji wanahitaji kupumzika."

# MOUKOKO AJIUNGA NA MARSEILLE




**MARSEILLE,** Ufaransa

MSHAMBULIAJI wa Borussia Dortmund, Youssoufa Moukoko ameamua kujiunga na Marseille kwa mkopo, ripoti imefichua.

Wakala wa mchezaji huyo hivi majuzi aliikashifu Dortmund kwa msururu wa ahadi zilizotimizwa ambazo zilimfanya Moukoko atamani kupeleka kipaji chake kwingine huku akitaka hatimaye kutimiza uwezo alioonesha katika soka la vijana.

Huku kukiwa na nia ya kutaka huduma yake kutoka England, Ufaransa na Hispania, Moukoko amechagua kuelekea Marseille, huku Fabrizio Romano akifichua kuwa mazungumzo kuhusu mkataba wa mkopo yanaendelea. Uhamisho wa Moukoko kwenda Marseille unatarajiwa kujumuisha chaguo la uhamisho wa kudumu msimu ujao wa joto.

Marseille wamekuwa wakifanya kazi katika soko la uhamisho wa majira ya joto. Baada ya kumsajili Roberto de Zerbi kama kocha wao mpya, timu hiyo ya Ufaransa tayari imeimarisha safu ya ushambuliaji kwa kumsajili Mason Greenwood kutoka Manchester United.

Kulikuwa pia na nia ya Marseille kumnunua Eddie Nketiah wa Arsenal.

Washikabunduki hao walikuwa wanataka karibu pauni milioni 30 kwa mshambuliaji wao huyo - ada ambayo inaweza kuwashawishi Marseille kutafuta mahali pengine. Licha ya dakika chache katika soka la wakubwa, Moukoko anajivunia rekodi ya kuvutia ya mabao.

Mabao 17 katika mechi 76 za Bundesliga kunaweza kusikovutia macho lakini ana wastani wa kufunga bao moja kwa dakika 140 za kucheza. Mkataba wa Moukoko na Dortmund bado una miaka miwili kukamilika.



# *Conor Gallagher akubali kutimkia Atletico Madrid*

**MADRID,** Hispania

CONOR Gallagher ametoa idhini yake ya kuhamia Atletico Madrid na jana Jumatatu alitazamiwa kusafiri hadi Hispania kukamilisha usajili wake na kuondoka Chelsea, kwa mujibu wa ripoti.

Baada ya kumuona Gallagher akiingia miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake, Chelsea ilikubali dau la euro milioni 40 kutoka kwa Atletico, lakini kulikuwa na sintofahamu kubwa iwapo kiungo huyo angekubali kuondoka.

Atletico walimwekea ofa Gallagher Jumapili na kuamua kufanya uamuzi na kama ilivyofichuliwa kwa mara ya kwanza na Fabrizio Romano, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 hatimaye amethibitisha nia yake ya kuhama.

Taarifa zaidi zinasema Gallagher alisafiri kwenda Hispania Jumatatu kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu na kukamilisha usajili wake kwa kikosi hicho cha kocha Diego Simeone.

Kiungo wa kati wa Celtic Matt O'Riley hivi majuzi alitajwa kama mbadala wa Gallagher huko Stamford Bridge.

Chelsea walikuwa wamempa Gallagher nafasi ya kusaini nyongeza lakini mhitimu huyo wa akademi hakufurahishwa na ofa ya mkataba wa miaka miwili, ambao pia ulijumuisha chaguo la miezi 12 zaidi.

Baada ya kumuona Gallagher akikataa nafasi ya kujiunga na Aston Villa, ambao walikuwa wamekubali kulipa ada kubwa kuliko Atletico, Chelsea ilimwonya Gallagher kwamba atashushwa kwenye kikosi B.

# Williams akataa kwenda Ufaransa

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Paris Saint-Germain imekiri kushindwa katika harakati zao za kumsaka nyota wa Euro 2024, Nico Williams, ambaye amekataa kuhamia Ufaransa msimu huu wa joto.

Williams amekuwa mmoja wa wahusika wakuu wa dirisha la usajili la majira ya kiangazi baada ya kuiongoza Hispania kutwaa ubingwa wa euro, huku Barcelona wakimtaka winga huyo wa Athletic Club.

Lakini hawako peke yao katika kumtamani mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22.

Miamba hao wa Ufaransa wamekuwa wakifuatilia mienendo yake lakini ripoti inadai kwamba, Williams hana nia ya kwenda kucheza Ligue 1.

Kukataliwa kwa PSG kutaonekana kuwa habari njema kwa Barca, lakini timu hiyo ya Katalunya bado inatatizika kwa ada sahihi ya kumpata winga huyo.

Rais wa Barcelona, Joan Laporta ameshutumiwa kwa kusema uwongo juu ya harakati zao za Williams na mgombea mshindani Victor Font, ambaye pia aliwaonya wafuasi kuhusu uaminifu wa Barca kushuka mwaka hadi mwaka.

Kocha wa Athletic, Ernesto Valverde, ambaye hapo awali alisimamia ushindi mara mbili wa taji la LaLiga na ushindi wa Copa del Rey kama kocha wa Barca, amefichua kuwa amepumzika kuhusu mustakabali wa Williams na hatazami ripoti za kila siku zinazomhusisha na kuondoka.

Barca hadi sasa wameshindwa kuongeza wachezaji wapya kwenye kikosi kilichomaliza nafasi ya pili nyuma ya Real Madrid katika Ligi Kuu ya Hispania.

Kiungo Dani Olmo ndiye anayelengwa zaidi, huku Barca ikifahamika kuwa wamewasilisha ofa kwa RB Leipzig ambayo ina thamani ya euro milioni 61.



HABARI MICHEZO

# KMC YAPANDISHA U20 WATATU LIGI KUU BARA

Na Adam Fungamwango

KLABU ya KMC imewapandisha wachezaji wake watatu wa kikosi cha vijana chini ya miaka 20 kwenye timu ya wakubwa na kuungana nao kwa msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Khalid Chukuchuku, amesema klabu hiyo imefanya hivyo kwa ajili ya kutambua umuhimu wa soka la vijana, pamoja na kuwapa chachu waliobaki na wengine wazidi kujituma kwani watakuwa wakiamini kuwa iwapo watafanya vyema basi watapandishwa kwenye kikosi cha kwanza.

**Waliopandishwa kwenye kikosi cha kwanza ni Shaaban Kimwaga, Karim Pongwe na Naseeb Majid, ambao sasa watatambulika kama ni wachezaji kamili wa KMC na kutarajia kucheza Ligi Kuu inayotarajiwa kuanza Agosti 16, mwaka huu.**

"Siyo kama tumewapandisha tu bali wameonesha uwezo mkubwa kwenye kikosi chetu cha vijana na hatimaye kocha amewasiliana na uongozi kuona uwezekano wa kuwapandisha, kwa sababu sisi zote tutataka kukuza soka la vijana, viongozi walikubaliana naye," alisema Chukuchuku.

Kikosi cha timu hiyo tayari kimesharejea Dar es Salaam kutoka Morogoro kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya msimu mpya wa mashindano, kikiwa pia kimefanya usajili wa wachezaji wapya, chini ya kocha Abdihamid Moalin, raia wa Somalia.

Wachezaji waliosajiliwa wa KMC kwa ajili ya msimu ujao ni kipa, Imasil Mpaki kutoka Biashara United, Ajoh Austin, straika kutoka Cameroon, Oscar Paul, kiungo mshambuliaji Mtanzania aliyekuwa akicheza soka la kulipwa nchini Kenya, katika klabu ya Kakamega Home Boys, beki wa kati, Nickson Kassam Mosha, akitokea kikosi cha vijana cha Mtibwa Sugar, kipa raia wa Burundi aliyekuwa akiidakia klabu ya Vipers ya Uganda, Fabien Mutombora, Jean Nyezimana kutoka Vital'O ya Burundi na beki wa kati, Salum Athumani 'Stopper' kutoka KVZ ya Zanzibar.

## Gamondi awavulia kofia wachezaji wapya

INATOKA UKURASA 24

Katika mchezo huo, Yanga ilishinda mabao 2-1, ikitanguliwa kufungwa bao la mapema dakika ya sita kupitia kwa Ricky Banda, lakini lilisawazishwa na Mudathir Yahaya dakika ya 64 na Stephane Aziz Ki akipachika bao kwa mkwaju wa penalti dakika ya 90.

Baada ya mchezo huo, Yanga inajiandaa na mechi ya Ngao ya Jamii itakayochezwa Alhamisi dhidi ya watani zao wa jadi, Simba kwenye Uwanja wa Mkapa, saa 1:00 usiku.

## Mutale awataka Yanga, Balua aahidi mabao

INATOKA UKURASA 24

Balua, aliyesajiliwa dirisha dogo la usajili akitokea Prisons, alisema msimu uliopita alifunga machache kutokana na kutokuwa chaguo la kwanza kwa makocha kwenye upigaji wa mipira iliyokufa.

"Nimefunga bao la mkwaju wa faulo katika mechi dhidi ya APR si kwa bahati mbaya, kwa sababu huwa nafanyia mazoezi kupiga mipira ya aina hii.

Msimu uliopita sikupiga sana kwa sababu ilikuwa ni mipango ya mwalimu kwani niliwakuta wapigaji wengi wazuri, ingawa na mimi nimeshafunga mabao ya aina ile, nilifanya hivyo na Namungo, wakati nipo Prisons niliifunga Simba, kwa hiyo si kitu kigeni sana.

Nawaambia mashabiki wa Simba tegemeeni mabao mengi ya faulo msimu huu, tunawashukuru sana kwa kujaza uwanjani, sasa wachezaji tunataka kuwalipa kwa kuwapa furaha," alisema.

Naye Awesu Awesu, aliyesajiliwa msimu huu akitokea KMC, alisema hatimaye ndoto yake imetimia, kwani alikuwa anataka siku moja awe mmoja wa wachezaji watakaotangazwa kwenye tamasha kubwa hilo, akiwa na kikosi cha Simba.

"Ni siku ambayo ilikuwa kwenye ndoto yangu, nilikuwa nafikiria na mimi kuwa mmoja wa watu watakaokuwa kwenye tamasha kubwa kama hili, nashukuru Mungu nimetimiza kwa kitu ambacho nilikuwa nakipenda.

Nilipotambulishwa hisia zangu nilikuwa kali sana, unajua kila mchezaji yoyote nchini anapenda kucheza timu kubwa kama hizi, narudia kusema hii ni ndoto niliyokuwa naisubiria maishani, kupambana kwangu kote nilikuwa nataka siku moja nicheze kwenye klabu ya Simba," alisema.

MNANISOMA?...



Mchezaji wa mpira wa Tennis, Rehema Selemani, akipiga mpira kurudisha kwa mchezaji mwenzake katika mazoezi yanayosimamiwa na Kocha Riziki Salum, walipokuwa wakifanya mazoezi katika Viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya maandalizi ya mashindano ya Kenya Open Championships mwezi huu, nchini humo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Nyoshi asema Bogoss ni chuo cha wanamuziki*

Na Sabato Kasika

MWIMBAJI nyota wa muziki wa dansi ambaye ni Rais wa Bendi ya Bogoss Musica, Nyoshi El-Sadat, amesema bendi yake ni chuo cha 'kupika' wanamuziki kisha wanachukuliwa na bendi nyingine.

Nyoshi alisema hayo jijini Dar es Salaam jana, kwamba tangu bendi hiyo ianzishwe zaidi ya miaka sita iliyopita, kuna wanamuziki wengi wamepita Bogoss na kuondoka huku wengine wakirudi kuendelea na kazi.

"Bogoss ni chuo cha wanamuziki kwani wakati ninaianzisha nilichukua wanamuziki wengi vijana wadogo na kukuza vipaji vyao, lakini wapo waliohama moja kwa moja, wengine wakarudi," alisema Nyoshi.

Nyoshi alisema, anajivunia kunyanyua vijana wengi kwenye dansi, na kwamba haoni tatizo mwanamuziki kuhama, kwa maelezo kuwa anatafuta vipaji vingine na kuviendeleza kwenye dansi.

"Wapo baadhi ya watu huwa wanachukia wanapoona wanamuziki wanahama kutoka katika bendi zao, lakini kwangu sio hivyo, mimi ninajisikia raha kuona kazi yangu inatangazwa zaidi," alisema.

Alifafanua kuwa, sehemu kubwa ya wanamuziki ambao amekuwa akichukua ni wa bongofleva, kwa maelezo kwamba wapo wenye vipaji, lakini anaamini muziki wanaoimba, baadhi yao hawawezi kupiga hatua.

Alisema muziki wa dansi unadumu zaidi, tofauti na huo wa bongofleva, na kwamba wale wanaoendelea kuimba muziki huo, baadhi yao sasa wameanza kuchanganya vionjo vya dansi kwenye nyimbo zao.

"Wamegundua kuwa dansi ina nguvu na inadumu, ndio maana wameanza kuchanganya, lakini nilionao kwenye bendi yangu ama nilioanza nao, ni wale walioamua kuacha muziki huo," alisema.

Michezo

Jumanne Agosti 6, 2024

Nipashe



Williams akataa kwenda Ufaransa UKURASA 22



Mshambuliaji wa Timu ya Yanga, Prince Dube, akikokota mpira mbele ya walinzi wa Red Arrows wakati wa mchezo wa kirafiki baina ya timu hizo uliochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi. Yanga ilishinda mabao 2-1. **PICHA: YANGA**

## Mutale awataka Yanga, Balua aahidi mabao

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya APR ya Rwanda, katika Tamasha la Simba Day, winga mchachari wa timu hiyo, Mzambia, Joshua Mutale (pichani), amesema wamesahau hilo na sasa akili na nguvu zote wanazielekeza katika mechi inayofuata dhidi ya Yanga.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Mutale, mmoja wa wachezaji wapya, waliosajiliwa msimu huu akitokea Power Dynamos ya Zambia, alisema baada ya kupata ushindi huo, wamekuwa na ari na kujiamini kiasi cha kutaka kuendeleza ushindi katika mechi ijayo ili kuwapa furaha mashabiki wao ambao walijitokeza kwa wingi Jumamosi kuwasapoti.



"Tumewaonyesha mashabiki ni kitu gani tunataka kufanya kuelekea msimu ujao, kizuri ni kwamba tumeanza kilele cha Simba Day kwa ushindi, na sasa tunaangalia mechi inayofuata dhidi ya Yanga, tunajiandaa na hilo na tutapambana," alisema winga huyo ambaye alionesha kiwango kikubwa katika mchezo huo.

Mchezaji huyo ameonesha kushangazwa na umati mkubwa uliojitokeza akisema ni kitu cha ajabu sana kukiona kwa macho.

"Ni kitu cha ajabu sana kwangu hiki nilichokiona, umati mkubwa kama ule, ulitufanya wachezaji kupambana uwanjani, kwangu ilikuwa ni mechi ya kwanza kubwa ya aina yake nikiwa na Simba," alisema Mutale.

Mfungaji wa bao la pili katika mechi hiyo, Edwin Balua, aliwaahidi wanachama na mashabiki wa timu hiyo kuwa msimu huu atafunga sana mabao ya faulo kuliko uliopita.

INAENDELEA UKURASA 23

# GAMONDI AWAVULIA KOFIA WACHEZAJI WAPYA YANGA

**Na Adam Fungamwango**

Asema wameelewa haraka kile anachokitaka kutoka kwao na...

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amewapongeza wachezaji wapya waliojiunga na timu hiyo msimu huu akisema wanaonekana kushika mafundisho yake haraka sana kuliko alivyotarajia.

Akizungumza juzi baada ya kumalizika kwa mechi ya tamasha la sita Wiki ya Mwananchi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Gamondi alisema wachezaji wapya wamezoea mazingira ya timu haraka sana, hivyo anaamini watakuwa msaada mkubwa kwa kikosi chake kwa msimu ujao wa mashindano.

"Tumefanya kazi kubwa na ngumu kuhakikisha tuko vizuri katika kile tulichokipata kwenye 'pre-season' yetu, ingawa hata hivyo matokeo ya mechi ya leo (juzi) siyo muhimu sana kwetu, kikubwa ni kuangalia tumecheza vipi, imekuwa ni rahisi sana kwa wachezaji wapya kuzoea mazingira ya timu na uchezaji, wamekuwa na wakati mzuri kwa kupokea kile ambacho nakiingiza kati yao, najivunia sana kwa hilo na nadhani watakuwa msaada mkubwa sana kwa timu kuelekea msimu ujao," alisema.

Wachezaji wapya ambao Yanga imewasajili ni Aziz Andambwile kutoka Fountain Gate, Clatous Chama akitokea Simba, Prince Dube aliyesajiliwa kutoka Azam FC, Jean Baleke kutoka Al Ittihad ya Libya na Duke Abuya akisajiliwa kutika Singida Black Stars.

Akizungumzia mechi yao waliocheza dhidi ya Mabingwa wa Dar Port Kagame Cup, Red Arrows ya Zambia, raia huyo wa Argentina alisema ilikuwa ngumu na nzuri, akiwasifu wapinzani wao kuwa wana kikosi bora na imara kinachoweza kufanya vyema katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

**Gamondi pia alisifu maandalizi ya nje ya uwanja ambayo yalionekana kuvutia kama kwenye mataifa makubwa katika soka duniani.**

"Ukiachana na hilo angalia tamasha lenyewe lilivyokuwa, kwa namna ambavyo uongozi ulivyoajiandaa, yanafanana na yale makubwa yanayofanyika, Argentina, Hispania na mataifa mengine makubwa kisoka, lakini kile ambacho kimetokea nje ya uwanja, maandalizi na burudani ni kitu ambacho hakielezeki, ni kizuri lakini ni faida kubwa kwa soka la Tanzania," alisema kocha huyo.

Kabla ya mechi hiyo, wasanii mbalimbali waliburudisha kabla ya kutangazwa kwa kikosi kipya cha msimu wa 2024/25.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >